tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#

Jumatano Oktoba 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581460 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Mchezo mchafu wauzaji mafuta

• **Malori** yatumia siku tano kusafirisha nishati hiyo umbali mfupi; EWURA yafungia vituo tisa... *Endelea ukurasa 2*




"Kuanzia Julai mwaka huu, kumekuwapo na matukio kwa baadhi ya maeneo, hasa pembezoni mwa nchi kukosa mafuta hasa kipindi bei zinapoelekea kubadilishwa na kusababisha kuwa na usumbufu...

**Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo**

## YALIYOMO

UKURASA WA 19

### OPERESHENI YA KUREKEBISHA MAUMBILE YAJA



HOSPITALI ya Taifa Muhimbili Tawi la Mloganzila, inatarajia kuanzisha huduma ya kurekebisha maumbile na...

## Samia aweka rekodi mwanamke kupewa shahada ya udaktari

UKURASA 3

# Waziri wa Elimu aijibu CHADEMA hoja uhalali mitaala mipya

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru, Prof. Santishree Dhulipudi Pandit, New Delhi nchini India jana. **PICHA: IKULU**

MICHEZO YANGA SC HAKUNA KULALA, NI TIZI TU UK.24 KATUNI UK.6

# Mchezo mchafu wauzaji mafuta

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imebaini mchezo mchafu katika uuzaji mafuta, ikivifungia vituo vingine viwili vya mafuta baada ya kubainika kuhodhi nishati hiyo.

Katika ufuatiliaji wake, EWURA imebaini baadhi ya wafanyabiashara wa nishati hiyo huficha kwenye malori na wengine kutumia mbinu ya kuyasafirisha mafuta kwa zaidi ya siku tano kwa maeneo yaliyoko na umbali mfupi.

Vituo hivyo vilivyofungiwa ni Kipenda Roho Investment Soya na Oilcom vilivyoko Soya wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma. Havitajihusisha na biashara hiyo kwa kipindi cha miezi sita huku EWURA ikisema vitendo hivyo ni miongoni mwa vinavyochangia bei ya bidhaa hiyo kupanda.

Kwa kipindi cha miezi tisa, bei ya nishati hiyo imepanda kwa takribani Sh. 400 hadi 600. Januari 4 mwaka huu, EWURA ilitangaza bei ya petroli kwa mwezi huo kuuzwa kwa rejareja kwa Sh. 2,819 na dizeli Sh. 3,295 kwa lita. Oktoba 4 mwaka huu, bei ya petroli kwa mkoa huo ikifikia Sh. 3,281 na dizeli Sh. 3,448 kwa lita moja.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, alitangaza adhabu hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam kuhusu sababu za bei ya nishati hiyo kupanda na hatua zinazochukuliwa, hasa zinazosababishwa na wafanyabiashara.

Jumla ya vituo tisa sasa vimefungwa kwa kuhodhi mafuta.

"Septemba 29 mwaka huu, EWURA ilivifunga vituo saba kwa miezi sita kwa makosa ya kuhodhi mafuta kinyume cha sheria. EWURA itaendelea na uchunguzi wa vituo vingine zaidi, ikiwa ni pamoja na kuwapa fursa ya kuwasilisha utetezi wao ndani ya siku 21," alisema Kaguo

Alisema hatua hiyo ilichukuliwa jana na Bodi ya Wakurugenzi wa EWURA baada ya uchunguzi kufanyika, akisema wamiliki hao wamebainika kwenda kinyume cha Sheria ya Petroli Sura Namba 392. EWURA inavitaka vituo kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji mafuta wakati wote.

"Kuanzia Julai mwaka huu, kumekuwapo na matukio kwa baadhi maeneo hasa pembezoni mwa nchi kukosa mafuta hasa kipindi bei zinapoelekea kubadilishwa na kusababisha kuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi na madhara ya kiuchumi.

"Pamoja na mafuta kuwapo nchini, changamoto ya upungufu wa mafuta katika maeneo mbalimbali, ilichangiwa na baadhi ya wamiliki wa vituo vya kuuzia mafuta kwa makusudi kabisa kuamua kuhodhi mafuta, kujipatia maslahi haramu ya kibiashara. Uamuzi huu sasa utakuwa umegusa vituo tisa," alisema.

Kaguo alisema bodi hiyo ilijiridhisha pasi na shaka kuwa vituo hivyo, vilitenda kosa la kuhodhi mafuta kati ya Julai na Agosti mwaka huu na hivyo imemua vifungwe kwa kipindi cha miezi sita.

"Baadhi yao waliyaficha katika magari ya mafuta na wengine wakitumia siku nyingi kuyasafirisha waendako wakati ni umbali mfupi na hata wakifika hawayauzi," alisema Kaguo.

Aliongeza kwamba EWURA inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisheria ikiwamo kuvifunga vituo vilivyothibitika kuficha mafuta kinyume cha kanuni na miongozo inayosimamia biashara ya mafuta nchini.

Septemba 16 mwaka huu, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, alipotembelea ofisi za EWURA, Dar es Salaam, alionya baadhi ya watumishi ambao wanajihusisha na vitendo vya kuvujisha siri za mamlaka hiyo siku chache kabla ya kutangazwa bei mpya kila mwezi.

Aliiagiza Bodi ya Wakurugenzi na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia upya kasoro zilipo, zinazosababishwa na watumishi hao na kujiridhisha iwapo wapo wasio waaminifu wabainishwe na kufundishwa namna ya kuwa waaminifu.

Septemba 18 mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu EWURA, Dk. James Andilile, alitangaza hatua walizoanza kuchukua baada ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Biteko, kutoa maagizo kuhusu suala la nishati hiyo nchini, akisema mifumo mitatu inarekebishwa ikiwamo ya uagizaji wa mafuta wa pamoja, upangaji bei na utoaji leseni.

"Sababu za upungufu wa mafuta baadhi ya mikoa, pamoja na kuwa na mafuta, baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakichukua mafuta na kuchelewesha kiyafikisha vituoni, huku wengine wakiwa na mafuta kwenye visima, lakini hawauzi na kusababisha kuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi," alisema.

Alisema serikali iliifanya sekta hiyo kuwa huria tangu miaka ya 1990 na si kuwa biashara holela, hivyo wafanyabiashara wafahamu wajibu utokanao na leseni pamoja na kutimiza haki ya huduma kwa Watanzania na si kukiuka masharti, kanuni na taratibu za leseni walizopatiwa.

Aliongeza kwamba EWURA inawapa onyo wafanyabiashara kwenye sekta hiyo kuzingatia leseni zao na kutoa huduma hiyo, akisema hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wanaokiuka sheria na haitasita kufunga biashara.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama (kushoto), akimsikiliza Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Baraka Ladislaus (kulia), alipotembelea banda la benki hiyo wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Vijana kitaifa, wilayani Babati mkoani Manyara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Waziri Elimu aijibu CHADEMA hoja uhalali wa mitaala mipya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amewajibu baadhi ya watu wanaodai hakuna ushirikishwaji katika maboresho ya sera na mitaala mipya ya elimu 2023.

Amesema maboresho hayo yameshirikisha watu wa aina zote na kuwatoa hofu wamiliki wa shule binafsi kwamba siyo maadui wala tatizo kwa serikali, bali wao ni fursa na wadau wenye msaada mkubwa katika sekta ya elimu.

Jijini hapa jana wakati wa kikao na wamiliki hao, Prof. Mkenda alisema mageuzi hayo yameshirikisha wadau na Rais aliagiza wasikilizwe watu wa aina zote hadi wanafunzi.

"Tulitangaza na rasimu ya mitaala ipo kwenye tovuti. Sasa ukisikia kuna watu wanasema maneno mitaala inataka kufundisha mambo ya ajabu, nenda kwenye tovuti kaangalie tu.

"Ninawahakikishia kwa rekodi zilivyo, kuna watu wanasema maneno fulani lakini walishiriki na walitia saini kwa sababu tulikuwa tayari kusikiliza mtu yeyote, wakatokea watu wakasema sisi mbona hatukusikilizwa wakaitwa," alisema.

Hivi karibuni, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kupitia Katibu Mkuu wake, John Mnyika, kiliwaambia waandishi wa habari jijini Dodoma kuwa hakijashirikishwa katika mchakato huo.

Prof. Mkenda serikali inahitaji ushirikiano na wamiliki wa shule binafsi na iko tayari kusikiliza maoni yao katika kuimarisha elimu nchini.

"Ninyi siyo maadui, ninyi siyo tatizo, ninyi si changamoto, ninyi ni fursa, ninyi ni wadau na ni msaada mkubwa kwa serikali huko tunakokwenda katika kuimarisha elimu na kwa sehemu kubwa mmepiga hatua na kutuonesha shule inatakiwa kuwa vipi kwa miundombinu mizuri na sisi tunajaribu kuiga humo humo," alisema.

Waziri alieleza kuwa serikali ina matendo yake itawaonesha namna inavyowahitaji ili kufanya kazi kwa pamoja.

"Ukiangalia wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na ukiangalia wanaoendelea kidato cha kwanza, takribani zaidi ya asilimia 20 ndiyo wanabaki nje hawaendelei, tumepiga hatua kubwa," alipongeza. Alisema ndoto za mageuzi ya elimu ambazo Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza zifanyiwe kazi, hazitatimia bila kufanya kazi na sekta binafsi.

Aliwaambia wamiliki hao mapendekezo yaliyomo kwenye mitaala kuwa ni pamoja na elimu ya awali ambayo ipo katika mabano, haijaamuliwa kama itakuwa ya lazima.

"Tutatamka ya lazima tutakapowekeza kwenye miundombinu na kila kitu na tuwe na uwezo wa kupokea kila mtoto anayeingia pale. Kuna 6:4:2/3+ ambayo kila mtoto lazima asome hadi kidato cha nne.

"Mapendekezo yaliyomo katika rasimu, elimu ya lazima ni miaka 10 ambayo kwa sasa ni miaka saba inajumuisha marudio mengi ambayo inaonekana kuchomoa ule mwaka wa saba ili aendelee na kidato cha kwanza hadi cha nne hapotezi kitu," alifafanua.

Alibainisha kuwa kwenye rasimu ya mitaala, wameondoa marudio ambapo elimu ya msingi ni miaka sita, lakini mwanafunzi haruhusiwi kukatisha masomo. Lazima akae shuleni miaka 10.

Kuhusu mafunzo ya amali, alisema kuna shule za michezo, kilimo na ufundi na kuomba sekta binafsi kuwekeza kwenye eneo hilo.

"Tunawahitaji sana kuwekeza kwenye mkondo wa mafunzo ya amali na tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuona tutawezeshaje ambao mtapenda kuanzisha mkondo wa mafunzo ya amali, hatutaanza kwa kasi kwa sababu kunahitaji uwekezaji, hatutaki watu wanyanyapae mafunzo ya amali kama yataanzishwa bila kuwekezwa vya kutosha.

"Tukisema shule ya michezo lazima kuwe na vitu vinavyohitajika na walimu wa michezo ili mtu akienda kusoma, ajue anapata elimu bora vinginevyo watakimbia upande mwingine.

"Ukienda mafunzo ya amali, kilimo lazima uwekeze, tunaomba mwekeze, mtuambie serikali ifanye nini," alisema Prof. Mkenda.

Kuhusu kalenda ya utekelezaji mitaala hiyo, waziri alisema kwa sasa wanaendelea na mchakato wa ngazi ya uamuzi kuthibitisha, hivyo utekelezaji wake utaanza Januari 2024.

"Tunaanzaje? Hatupigi kwa mkupuo hatutofanya 'big burn'. Tukifanya big burn, hatari yake tutaharibu mfumo wa elimu wa nchi yetu.

"Mapendekezo yanayojadiliwa leo na yatakayopita hivi karibuni, yakipita yalivyo bila marekebisho yatakuwa kwanza kidato cha kwanza na elimu ya awali wataanza na mitaala mipya," alisema.

Alisema maandalizi yapo, watafundisha walimu wa shule za umma na binafsi.

"Serikali itakaa nao na kuwapitisha kwenye mitaala hiyo ili tuweze kuanza, halafu ili tusichelewe sana kuja kufanya mageuzi tutaingia tena darasa la tatu.

"Kwa hiyo, tutaanza na mitaala mipya kwa pre-school (elimu ya awali), darasa la kwanza hadi la tatu mitaala mipya, kidato cha kwanza mitaala mipya, kidato cha tano mitaala mipya halafu elimu ya ualimu mwaka wa kwanza mitaala mipya," alifafanua.

Aliongeza kuwa vitabu vya kiada na ziada ni muhimu, kikubwa kuandaa walimu.

Naibu Waziri wa Elimu, Omar Kipanga, alisema kikao hicho kinalenga kujadili changamoto zinazowakabili na kutafuta namna ya kuzitatua ili kufanya kazi kwa pamoja na kuleta tija kwa taifa.

HABARI KITAIFA

# Samia avunja rekodi shahada udaktari

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameweka historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kutunukiwa Shahada ya udaktari wa heshima na Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru, New Delhi, India kwa kutambua mchango wake katika kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na India.

Shahada hiyo pia imetolewa kwa kutambua mchango wake wa kuboresha maisha ya Watanzania na mafanikio yake kikanda na kimataifa na kukuza diplomasia ya uchumi.

Akipokea shahada hiyo ambayo ni ya kwanza kwake kutoka ugenini jana, Rais Samia alikishukuru chuo hicho kwa heshima hiyo kubwa na kuielekeza kwa watoto wa kike wa Tanzania wanaoishi katika mazingira magumu.

Rais alisema ameitoa tuzo hiyo kwa watoto hao kutokana na mazingira halisi aliyopitia tangu akiwa shule ya msingi hadi kufikia nafasi aliyo nayo sasa na mchango wa wazazi wake ulivyochangia kumfikisha hatua hiyo.

Aliwasihi watoto wa kike kutokata tamaa kutokana na mazingira waliyomo na kuitaka jamii kushirikiana kuwawezesha watoto hao kufikia ndoto zao kama ambavyo wazazi wake walimshika mkono katika kipindi chote cha kuzifikia ndoto zake.

"Shahada hii inanikumbusha mbali nikiwa mtoto mdogo nikienda shuleni katika kijiji nilichozaliwa cha Kizimkazi huko Unguja, Zanzibar, mama yangu akiwa mama wa nyumbani na baba mwalimu. Nawashukuru kwa kunipatia muda ulioniwezesha kufikia ndoto zangu za elimu, siasa na hatimaye kufikia nafasi niliyo nayo sasa," alisema.

Pia aliwashukuru viongozi waliomtangulia kwa kumwandalia njia na mwongozo mzuri ambao anautumia kuendelea kuipeleka nchi eneo salama, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Watanzania kwa mchango wao uliomwezesha kufikia hatua hiyo muhimu katika maisha.

"Ninafahamu kabisa kwamba chochote ninachopata kama kiongozi wa nchi yangu, kwa kiasi fulani ni kwa sababu ninasimama kwenye mabega mapana ya kaka zangu, watangulizi wangu ambao wamejitolea maisha yao katika kuifanya taasisi ya urais kuwa yale niliyorithi.

"Mchango wa India kwa maendeleo ya Tanzania ni mkubwa. Matokeo ya ushirikiano wao yanaonekana katika biashara. Ikiwa mshirika namba nne wa biashara nchini na kusababisha biashara baina ya nchi hizo kukua kutoka dola bilioni 2.6 mwaka 2017/2018 hadi dola bilioni 6.5 mwaka 2022/2023," alisema.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru, Santishree Pandit, alisema anajisikia heshima kubwa kumtunuku Rais Samia udaktari wa heshima kwa mchango wake wa kuboresha uhusiano kati ya Tanzania na India, mafanikio yake kikanda na kukuza diplomasia ya uchumi.

Alisema rais huyo ni kiongozi wa pili kutoka Tanzania kutunukiwa shahada hiyo kwa kuwa mwaka 1995 chuo hicho kilimtunuku shahada kama hiyo Hayati Julius Nyerere.

Chuo hicho, alisema ni moja ya vyuo 10 kwa ubora duniani katika masomo matano na kimetoa washindi wawili katika tuzo za Nobel wote wakitokea katika uchumi.

Waziri wa Mambo ya Nje wa India, Subrahmanyam Jaishankar, alisema Rais Samia ni kiongozi wa kwanza wa Afrika kuitembelea nchi hiyo tangu Umoja wa Afrika (AU) ulipoingizwa katika mataifa yaliyoendelea kiviwanda duniani (G20).

Alisema moja ya vipaumbele katika ushirikiano wa nchi hizo ni elimu na kujengea wananchi uwezo, hivyo zaidi ya Watanzania 5,000 wamepata mafunzo katika taasisi za elimu za India hasa kwenye teknolojia.

Pia alisema nchi hiyo imeamua kuanzisha Taasisi ya Teknolojia ya India Zanzibar yenye fursa ya kuwa kituo kikuu cha elimu ya teknolojia barani Afrika.



## Shekhe mshtakiwa wa utapeli aangua kilio akiwa kizimbani

**Na Grace Gurisha**

SHEKHE Rashid Kisuguru (53), maarufu kama Shekhe Sharifu wa Makarama, anayetuhumiwa kujipatia Sh. milioni 54 kwa njia ya udanganyifu kwa madai kuwa atampa muumini wake utajiri kwa njia ya miujiza, ameangua kilio mahakamani akiomba apunguziwe masharti ya dhamana.

Aidha, amedai kuwa familia yake imefukuzwa kwenye nyumba baada ya kodi kwisha na pia mke wake amejifungua mtoto njiti.

Shekhe Kasuguru alilitoa ombi hilo huku akilia mbele ya Hakimu Mkazi Ramadhani Rugemalira wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Kinondoni, Dar es Salaam, baada ya kumaliza kusomewa maelezo ya awali ya shtaka linalomkabili.

"Mheshimiwa naomba mahakama yako tukufu inipunguzie masharti ya dhamana. Familia yangu imefukuzwa kwenye nyumba baada ya kodi kwisha na pia mtoto wangu amezaliwa njiti," alidai huku akilia ndani ya kizimba cha mahakama.

Hata hivyo, Hakimu Rugemalira alimhoji kwamba kwa nini analia kwamba amenyimwa dhamana na mahakama? Mshtakiwa alidai kuwa hajanyimwa dhamana lakini shida ni hati ya nyumba ya Sh. milioni 50.

"Shida si mahakama ni sheria ambazo zimetungwa. Kwa hiyo mahakama inafuata hizo, yaani unachoniomba ni kwamba mimi nivunje sheria ambayo imetungwa kwani nusu ya fedha hiyo ni shilingi ngapi?" Alisema Hakimu Rugemalira.

Shekhe Kasuguru alidai kuwa dhamana hiyo nusu yake ilikuwa Sh. milioni 27, kwa hiyo inatakiwa hati ya nyumba ya kiasi hicho ndiyo maana aliomba apunguziwe.

"Kwa hiyo unataka nivunje sheria? Sasa Shekhe hata hapa mahakamani wadhamini wako hawapo, walete wakudhamini si kubadilisha masharti ya dhamana," alisema Hakimu.

Akisoma maelezo hayo, Wakili wa Serikali, Rhoda Maingu, alidai kuwa mshtakiwa, mkazi wa Sinza, anadaiwa kati ya Agosti na Septemba, 2022 akiwa Kawe na Sinza, alijipatia Sh. milioni 54 kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa muumini wake, Said Mchana.

Ilidaiwa kuwa Sheikh Kasuguru alijipatia fedha hizo kwa madai kuwa atamfanya muumini wake utajiri kimiujiza huku akijua si kweli na kwamba walijuana hadi kufikia hatua hiyo kwa sababu alikuwa muumini wake.

Wakili Maingu alidai mshtakiwa alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi Oysterbay na kuhojiwa ndipo Septemba 26, 2023 alifikishwa mbele ya mahakama kujibu mashtaka yanayomkabili.

Baada ya kusomwa maelezo hayo alikubali anwani zake za makazi na majina yake lakini maelezo mengine aliyakataa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Oktoba 24, mwaka huu kwa kutajwa hakimu alimweleza mshtakiwa kuwa akipata wadhamini hata kesho atadhaminiwa kwa sababu dhamana iko wazi.


CHAMA CHA WALIMU TANZANIA
CWT
WAJIBU NA HAKI

**Tender No. TTU/T/C/2023/2024**
**for**
**Supply and Distribution of T-shirts and Caps**

**Invitation for Tenders**

**Date: October 11, 2023**

1. This Invitation for Tenders follows Tanzania Teachers' Union, which appeared in Tanzania Teachers' Union financial regulations 3rd Edition of 2018.
2. Tanzania Teachers' Union has set aside funds for supply and Distribution of T-shirts and Caps during the financial year 2024.
3. Tanzania Teachers' Union now invites tenders from eligible Supplier to Supply and Distribute T-shirts and Caps.
4. Tendering will be conducted through the National Competitive Tendering method specified in Tanzania Teachers' Union Financial Regulations 3rd edition of 2028.
5. Interested eligible Tenderers may obtain further information from, inspect the tendering document physically at Tanzania Teachers' Union, and pay tender participation of non-refundable fee of Tanzania Shillings 500,000. Payment is performed through bank via account National Microfinance Bank (NMB) 20101300312 Name Tanzania Teachers' Union and collect set of Tendering Documents physically at Tanzania Teachers' Union Head quarter office, Jamhuri Stadium from 8:00 AM to 10:00 PM (Monday to Friday).
6. A Tender Securing Declaration in the format provided in the tendering document must accompany all tenders.
7. All Tenders must be physically submitted in the proper format, at or before 26/10/2023, 09:59AM. Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend at TTU-Head quarter office, ground floor meeting room, Box 3077, Jamhuri Stadium Dodoma.

General Secretary
Tanzania Teachers' Union-TTU
P.O.BOX 3077
DODOMA

THE SECRETARY GENERAL
TANZANIA TEACHERS' UNION (TTU)
DODOMA - HEADQUARTERS

# Mwinyi awahakikishia maendeleo wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itahakikisha huduma bora za kijamii na kiuchumi, kukuza uchumi endelevu na kupambana na umaskini kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana visiwani humo wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa Umoja wa Mashirika ya Utangazaji wa Umma Kusini mwa Afrika (SABA).

Alisema ndio maana imeweka dira ya mazingira wezeshi ambayo yatachochea na kukuza uchumi wa kasi kwa kuwa na ushirikiano na nchi nyingine, kushirikisha sekta binafsi pamoja na kuhakikisha uwekezaji katika sekta ya TEHAMA unaongezeka.

Aidha, lazima kuhakikisha kuwa sekta ya habari na utangazaji zinakuwa nyenzo ya kutoa taarifa sahihi kwa wananchi, ili kuimarisha utulivu na amani na hivyo kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na wananchi.

"Sote ni mashahidi wa namna vyombo vya utangazaji na habari vikiwamo vyombo vya umma vya utangazaji vya nchi zetu za Afrika vilivyo na umuhimu mkubwa katika kutoa taarifa zinazochangia maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kujenga amani, utulivu, usalama na utengamano wa nchi zetu," alisema.

Dk. Mwinyi alisema lazima nchi ijipange kuwa tayari kwenda na mabadiliko, kwasababu wakati utalazimisha kubadilika na athari ya kusubiri kubadilishwa na wakati zinaweza kuwa hasi na pengine kufanya mashirika ya utangazaji ya umma kupoteza mvuto kwa umma.

Aidha, alitoa rai ya kuendelea kufanya uwekezaji katika mashirika ya utangazaji kwa kuwezeshwa kuwa na vitendea kazi vya kisasa vinavyoendana na maendeleo na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani.

"Msisitizo wa kukuza uchumi wa kidijitali na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano haitoacha nyuma sekta ya utangazaji hivyo mashirika yetu ya utangazaji ya TBC na ZBC nayo pia yanashirikishwa katika mpango huo wa nchi kwenye maendeleo ya TEHAMA na mchango wake katika ukuaji wa uchumi wa kidijitali nchini kwetu kwa maendeleo endelevu," alisema.

Dk. Mwinyi alikumbusha nafasi ya vyombo vya habari ikiwamo radio, televisheni na mitandao ya kijamii katika ukuaji wa uchumi, utengamano wa kitaifa pamoja na ustawi wa kisiasa wa nchi hususan zilizopo Kusini mwa Afrika, hivyo lazima kuwa wabunifu. "Pia nimejulishwa kwamba kupitia mkutano huu pamoja na mada kuhusu TEHAMA mtajadiliana kuhusu mada nyingine mbalimbali hivyo napenda kutoa wito kwenu nyote, mshiriki katika mijadala hiyo kwa hoja zitakazosaidia kuweka mbele maslahi ya watu na nafasi ya Bara la Afrika katika kuandaa na kutangaza habari zinazolenga kuleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kiutamadumi na utengamano wa kijamii," alisema.

Rais wa Jumuiya ya Vyombo vya Habari vya Umma Kusini mwa Afrika (SABA), Stanley Similo, alisema ni muhimu kuzingatia kusonga mbele na sio kurudi nyuma katika kuendeleza vyombo vya habari vya umma na hatua iliyofikiwa.

Alisema vyombo vya habari vya umma vinakwenda vizuri na hakuna kurudi nyuma katika safari hiyo mpaka sasa, huku kuna haja ya kuzingatia tunapoangalia habari za upotoshaji, kila tunapoangalia wapi pa kwenda na wapi pazuri kwa kila mwananchi.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Tanzania, Kundo Mathew, alisema vyombo vya habari vina jukumu la kusukuma ajenda ya habari inayosisitizwa katika mkutano huu wa SABA, kwa kuwa vyombo vya habari vina jukumu la kuhakikisha jamii inapata taarifa na kuhabarishwa.

Alisema ni muhimu kuwa na ajenda maalumu na kutembea kwa pamoja katika hizi nchi za Afrika ili kwa pamoja kusukuma gurudumu la maendeleo katika nchi zote za Afrika.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 30 wa Vyombo vya Utangazaji vya Umma Kusini mwa Afrika (SABA), Kiembesamaki, Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: IKULU**

## Maradhi afya akili yapungua Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TAKWIMU za magonjwa ya afya ya akili kwa Mkoa wa Dodoma zinaonyesha kupungua kutoka asilimia 35 hadi 31 huku kifafa kikiongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Nelson Bukuru, alisema hayo jana jijini hapa kwenye maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani.

Alisema kwa mujibu wa takwimu ya mwaka 2020 hadi 2022, mkoa wa Dodoma unaonyesha magonjwa hayo yamepungua kwa asilimia 35 hadi kufikia asilimia 31.

"Kupungua kwa magonjwa haya ya afya ya akili bado kwa mkoa wetu wa Dodoma kuna tatizo la kuongoza kwa wagonjwa wa kifafa. Kwa mwaka 2022 kati ya wagonjwa 24,183 wa magonjwa ya afya ya akili, kati yao 19,000 sawa na asilimia 79 walikuwa wa kifafa," alisema.

Aidha, alisema kupungua kwa magonjwa hayo ya afya ya akili inatokana na kuongezeka kwa watumishi katika Hospitali ya Mirembe pamoja na elimu inayotolewa kwa wanajamii ili kujitahadharisha na magonjwa hayo.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema afya ya akili ni tatizo la kila mtu na ili kumaliza, ni lazima kushikamana na si kuwatenga wala kuwanyanyapaa watu wenye tatizo hilo.

Aliwataka watumishi wa afya wanaohudumia waathirika wa magonjwa ya afya ya akili kuhakikisha wanatoa tiba sahihi.

Pia alisisitiza mfumo utakaowawezesha kutambua watu hao ambao wana dalili na tatizo hilo ili kuwapa kipaumbele kwenye hospitali na kupatiwa dawa sahihi.

Naye Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Saitore Laizer, alisema serikali itaelekeza nguvu kuifikia jamii katika kukabiliana na magonjwa hayo na kuondoa hofu kwa wananchi.

Alisema elimu hiyo ikitolewa itaondoa na kupunguza kwa idadi ya wagonjwa na kutoa wito kwa wataalamu wa afya hiyo kuelimisha jamii juu ya magonjwa hayo.

"Hata hivyo bado kwa upande wa malezi ya kwenye familia na wazazi pia imekuwa ikichangia kusababisha ugonjwa huo kutokana na walio wengi kujihusisha kwenye matumizi ya dawa za kulevya, unywaji wa pombe za kupindukia," alisema.

## Tanzania yaahidi kukuza ushirikiano katika miradi ya kimkakati na Uganda

**Na Neema Mbuja,**
KAMPALA

TANZANIA imeahidi kuendeleza ushirikiano na Umoja katika miradi ya kimkakati kwenye sekta mbalimbali kwa manufaa ya nchi zote mbili.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayo juzi wakati akiwasilisha salamu za Rais Samia Suluhu Hassan kwenye maadhimisho ya miaka 61 ya uhuru wa Uganda yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Kitgum, kaskazini mwa nchi hiyo. Akitoa salamu hizo, Dk. Biteko alisema Rais Samia anathamini mchango na maendeleo yaliyofikiwa na Uganda katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kiuchumi.

"Mheshimiwa Rais anakupongeza sana kwa siku hii muhimu ya miaka 61 ya uhuru na wananchi wote wa Uganda na ameahidi kuendelea kishirikiana katika kujenga uchumi wa nchi hizi mbili na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Aidha, Biteko alisema Rais Samia anamshukuru Rais Yoweri Museveni kwa jitihada zake za kudumisha umoja na mshikamano kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tanzania na Uganda zimekuwa na uhusiano na ushirikiano wa muda mrefu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kiuchumi ikiwamo miradi ya kimkakati ya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda mpaka Tanga pamoja na miradi mbalimbali katika sekta za nishati, utalii na kilimo.

Historia ya Tanzania na Uganda ilianza tangu kipindi cha harakati za uhuru baina ya waasisi wa nchi hizo na ushirikiano huo unaendelezwa na kudumishwa kwa umoja, amani, mshikamano na utu uliopo baina yao.

Maadhimisho ya miaka 61 ya uhuru wa Uganda yalihudhuriwa na Makamu wa Rais Burundi, Prosper Bazombanza, wawakilishi kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Peter Mathuki, mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao nchini Uganda, mawaziri, wabunge kutoka Uganda na wananchi.

**TANGAZO**

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE
## REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY (TARURA)

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY
TARURA
Improved Roads For Sustainable Development

**P.O. BOX 11042,**
**DODOMA.**

# REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI)
## (CONSULTING SERVICES – QCBS SELECTION)

| | | |
|---|---|---|
| **Country** | : | **Tanzania** |
| **Name of Project** | : | **Tanzania Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities (RISE) Project** |
| **Credit No.** | : | **IDA-68670 - TZ** |
| **Assignment Title** | : | **Consultancy services for the Establishment, Registration and Administration training of Community-Based Routine Maintenance (CBRM) Groups** |
| **Reference No** | : | **AE.092/WB-RISE-P164920/375917/2023/24/C/03** |

This request for expression of interest follows the General Procurement Notice for this Project that appeared in the United Nations Development Business (UNDB) No. WB-P164920 of December 14th December, 2021

The Government of the United Republic of Tanzania through Tanzania Rural and Urban Roads Agency (TARURA) and Tanzania National Roads Agency (TANROADS) has received a credit from the International Development Association (IDA) towards the cost of Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities (RISE). It is intended that part of the proceeds of the credit will be used to cover eligible payments under the contracts for Consultancy services.

The consulting services ("the Services") is the establishment, registration and administration training of Community-Based Routine Maintenance (CBRM) Groups, allowing these CBRM Groups to be subsequently (sub)contracted by TARURA for routine road maintenance.
Specifically, the Consultant will: (i) Carry out the identification and selection of CBRM Group members from communities along the roads to be maintained, (ii) Register the CBRM Groups in line with organizational modalities approved by TARURA, and (iii) Train the established CBRM Groups with regards to group administration and (sub)contract implementation. The total duration for the entire assignment shall be about **Eight 8 calendar months** from contract effective date.

The detailed Terms of Reference (TOR) is attached to this request for Expression of Interest and is also available at TARURA's website www.tarura.go.tz. All requests for clarification should be sent through office email pmurise@tarura.go.tz and the Client will respond to the requested clarifications. The Consultants would be responsible for ensuring that any addenda available on the website is also downloaded and incorporated

The Chief Executive TARURA, now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the above services. Interested consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services. The shortlisting criteria are:

A. Core business and 10 years in business.
B. Relevant similar experience, which should specifically include the below:
    i) Experience of at least two (2) similar assignments completed in the past 5 years. Information to be provided should include name of assignment, name and full contact address of the client, contract value (in equivalent US dollars) and period (dates) of execution of assignment and the role played in the assignment (Lead or JV partner)
    ii) Demonstration of experience of work in similar conditions.
C. Technical and Managerial Capability of the firm (Provide only the structure of the organization, general qualifications and number of key staff). Do not provide CV of the staff. Experts will not be evaluated at the shortlisting stage).

The attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" Fourth Edition, November 2020 ("Procurement Regulations"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

Consultants may associate with other firms to enhance their qualifications but should indicate clearly whether the association is in the form of a joint venture and/or a sub-consultancy. In the case of a joint venture, all the partners in the joint venture shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected. Therefore, each member of JV shall independently meet the requirements of the evaluation criteria. The experience, technical & managerial capability of the Sub-Consultant shall not be evaluated to enhance the qualification of the Lead Firm or JV.

A Consultant will be selected in accordance with the ***Quality and Cost Based Selection (QCBS)*** method set out in the Procurement Regulations.

Further information can be obtained at the address below during office hours from **08.00 to 17.00 hours Local time Monday to Friday** except public holidays.

Expressions of interest must be delivered in a written form to the address below in person, or by e-mail ***pmurise@tarura.go.tz by 25th October, 2023 1430 Hours East African Time.*** The firms that will submit their EOI via e-mail must get confirmation of the receipt of their documents. In case the firm does not receive acknowledgement within two days of after sending the documents via email they should **call +255752460018/+255759348494/+255622759393** for follow-up.

***The address referred above is:***
***The Secretary, TARURA HQ Tender Board***
***Street Address: Mtaa wa Kazi 41207 Mtumba,***
***Building: TARURA House***
***Address: P.O. Box 11042, Dodoma, Tanzania.***
***Floor/ Room number: Ground Floor/PMU Office***
***City/Town: Mtumba Government City Area***
***Country: United Republic of Tanzania***
***Telephone: +255752460018/+255759348494/+255622759393***
***Electronic mail address: pmurise@tarura.go.tz***

217640902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ziara ya Rais Samia India yaonesha nuru

**RAIS** Samia Suluhu Hassan yupo nchini India kwa ziara ya kitaifa ambapo nchi hizo mbili zimekubaliana kuimarisha ushirikiano kwenye maeneo ya kimkakati kwa manufaa ya pande zote yakiwamo maji, kilimo, teknolojia, afya, ulinzi na usalama, utamaduni na michezo, uchukuzi, biashara na uwekezaji.

Alipokutana na Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, Rais Samia aliipongeza serikali ya nchi hiyo kwa kuendelea kuwa mshirika muhimu na kuchangia maendeleo ya Tanzania hususan kwenye maeneo ya kimkakati.

Maeneo ya kimkakati yaliyotajwa yanaleta nuru ya kuwapo kwa maendeleo makubwa nchini hasa ikizingitiwa ushirikiano uliopo kati ya nchi hizo mbili.

Uamuzi huo ni heshima na upendeleo kwa Tanzania kwa kuwa utawanufaisha Watanzania, Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla.

Ziara hiyo ya Rais Samia ni dhahiri kuwa ushirikiano wa nchi hizo umeongeza thamani ya ufanyaji biashara na takwimu zinaonyesha kuwa biashara imeongezeka.

Kwa mujibu takwimu hizo biashara imeongezeka hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.1 mwaka 2022 kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2017.

Rais Samia pia aliipongeza India kwa kufanikiwa kuandaa Mkutano wa G20 ambapo Waziri Mkuu Modi ameitetea Afrika kuwa mwanachama kamili wa G20, mpango wa kupunguza madeni kwa mataifa madogo na kutangaza mpango wa dharura wa kuhamasisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya nchi zinazoendelea ili kuwezesha upatikanaji wa teknolojia ya nishati safi ifikapo mwaka 2050.

Tanzania na India zimekubaliana kukuza ushirikiano uliopo katika viwango vya juu vitakavyowanufaisha wananchi wa mataifa hayo.

Kwa Tanzania itanufaika kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya kutokana na nchi ya India kufanya vizuri kwenye sekta hiyo ambapo wagonjwa walioshindikana kwenye nchi zao (si Tanzania pekee) kuwa na uhakika wa matibabu mazuri nchini humo.

Tanzania na India pia zimekubaliana kuwa na mpango wa miaka mitano wa ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama hususan katika maeneo ya kujenga uwezo, mafunzo na ulinzi baharini.

Jambo la kufurahisha zaidi ni makubaliano ya nchi hizo kutumia sarafu za nchi zao kukuza na kuongeza biashara na kupunguza gharama na matumizi ya Dola za Marekani.

Viongozi hao pia walishuhudia ubadilishanaji wa hati sita za makubaliano ya ushirikiano baina ya mataifa yao katika sekta za uchukuzi, utamaduni, michezo, uwekezaji, TEHAMA na afya.

Baadhi ya hati hizo ni makubaliano kati ya Wizara ya Elektroniki na Teknolojia ya Habari ya India na Wizara ya Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari ya Tanzania kuhusu ushirikiano wa kupeana suluhu zenye mafanikio za kidijitali zinazotekelezwa kwa ujuzi wa idadi ya watu kwa ajili ya mabadiliko ya kidijitali.


Nyingine mabadilishano ya hati ya makubaliano ya kiufundi kati ya Jeshi la Wanamaji la India na Shirika la Wakala wa Meli wa Tanzania (TASAC) kuhusu kupeana taarifa za meli za kibiashara.

Nchi hizo pia zilitia saini makubaliano ya mpango wa kubadilishana utamaduni kati ya India na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka ya 2023 hadi 2026.

Pia hati ya makubaliano kati ya Mamlaka ya Bandari ya Jawaharlal Nehru chini ya Wizara ya Usafirishaji wa Bandari na Njia za Majini ya India na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa ajili ya kuanzisha bustani ya viwanda nchini Tanzania.

Kamishna wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) chini ya Wizara ya Fedha, David Kafulila, alisema kupitia ziara hiyo atakwenda kujifunza mambo mengi hasa namna nchi hiyo ilivyojikomboa kiuchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Haya ya Simiyu yakome, ni aibu

**KINACHOWEZA** kuelezwa kutokana na yaliyowakuta mapacha Pendo na Furaha Saku, ni hiki. Ndoa za utotoni na kuamini waganga wa jadi kwenye mikoa ya kanda ya ziwa ni fedheha kwa taifa.

Mapacha hao wanaotoka Bariadi mkoani Simiyu wamefariki dunia kwa kile kinachodaiwa kuwa kimesababishwa na kupakwa dawa ya asili ili kukuza matiti tayari kwa kuozwa.

Wasichana hao waliomaliza kidato cha nne wakiandaliwa kwenda chuo cha ufundi walipelekwa kwa mganga ili kufanyiwa tiba hiyo ambayo iliwaumiza na kusababisha kuhara na kutapika damu na kupoteza maisha wiki iliyopita Oktoba 4.

Mikoa ya ukanda huo ikiwamo Shinyanga pamoja na jirani yake Simiyu ni miongoni mwa maeneo ambayo kuozesha watoto ndoa za udogoni limeota mizizi hata kusababisha kuwaharibia ndoto zao kielimu na maisha kwa ujumla.

Mabinti kwenye ukanda huo wanaozeshwa wakiwa wadogo, wengine kupelekwa kushiriki kwenye ndoa za kimila ziitwazo 'bukwilima' ili kujamiiana na wanaume wanaomsindikiza bwana harusi ikiwa ni njia ya kuwatafutia wanaume wa kuwaoa.

Lakini, kuna masuala mengine kama wazazi na walezi kuwaogesha watoto hao dawa za mvuto wa mapenzi, yote hayo yakiwatumbukiza mabinti kwenye maangamizo mapema.

> **Lakini, kuna masuala mengine kama wazazi na walezi kuwaogesha watoto hao dawa za mvuto wa mapenzi, yote hayo yakiwatumbukiza mabinti kwenye maangamizo mapema.**

Kilichotokea Simiyu hadi mabinti hao kupoteza maisha ni jambo linalohitaji nguvu ya kuwaondoa watu wengi kwenye giza la kuendelea kuoza watoto wadogo na pia kufanya mbinu za kuwakuza mfano kuongeza ukubwa wa matiti.

Kuna haja ya taifa sasa kuamka na kupambana na adui ujinga ndani ya jamii hizo ambazo zimekuwa na mikasa ya ajabu inayoangamiza maisha ya watu, mathalani mikoa ya Kanda ya Ziwa ndiyo iliyoanzisha mauaji ya watu wanaoishi na ualibino.

Ushirikina na ibada za matambiko na kuendekeza mila potofu kuwa utajiri unapatikana kwa kuua wenye albinism nakutumia viungo vyao ili kupata mali ulitikisa dunia hadi Tanzania kuonekana kama adui wa kundi hilo.

Serikali ilikomesha mauaji hayo, lakini ikumbukwe kuwa pamoja na kuua albino mikoa hiyo ni maarufu kuchinja kikatili na kuu wazee. Vijana na watoto wakiwaua wazazi wao hasa wanawake kwa kisingizio kuwa ni wachawi.

Mikoa hiyo inahitaji kampeni za kitaifa za kuelimisha familia kuwa si wakati wa kuoza watoto wa kike, si zama za kukuza viungo vya mwili ili kuharakisha ndoa wala siyo muda wa kuamini uganga na ushirikina kwa vile athari zake wameziona.

Inavyoelekea zinahitajika nguvu zaidi kuanzia ndani ya vijiji, shuleni, kwenye ibada, zinapotolewa huduma za kijamii hospitalini, vyuo vya elimu, kwenye uzalishaji hasa magulioni, sokoni kwenye minada na kila kwenye kusanyiko, ili umma uelimishwe kuachana na mila na desturi zinazoangamiza maisha ya watoto, mabinti, wenye ulemavu na wazee.

Ni vyema pia kuwapo na sheria ndogondogo za kukataza mila hatarishi kama bukwilima, lakini ziwepo za kusimamia tiba za jadi, nyingine zitungwe kuzuia ngoma na mila zinazowaangamiza wasichana na za kuwabana wazazi na walezi wanaokwamisha watoto wa kike kusoma.

Ifike kipindi sheria hizo zipige marufuku ndoa kufungwa bila ya kupata kibali cha serikali iwe ya kijiji, mitaa, kata na polisi.

Viongozi wa serikali kuanzia wabunge na wanasiasa wahamasishe na kufuatilia mabadiliko ili kukomesha matukio yanayoua watu ndani ya jamii hizo ambayo sasa yanafikia hatua ya kuliaibisha taifa.

Ikiwezekana mashuhuda au waathirika wa madhara ya kuozeshwa ndoa za utotoni wawezeshwe watembelee wananchi na kueleza kilichowasibu na pia wale waliopoteza watoto wao wapewe vipaza sauti majukwaani kuushuhudia ukweli, juhudi zilenge kuokoa kwa vile hatua iliyofikiwa inakatisha tamaa.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY (TARURA)

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY TARURA Improved Roads For Sustainable Development

P.O. BOX 11042,
DODOMA.

# REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI)
# (CONSULTING SERVICES – QCBS SELECTION)

**Country:** **Tanzania**
**Name of Project:** **Tanzania Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities (RISE) Project**
**Credit No.:** **IDA-68670 – TZ**
**Assignment Title:** **Consultancy Services on ICT Assessment and Development of Digital Transformation Road Map to TARURA**
**Reference No.:** **AE.092/WB-RISE-P164920/374435/2023/24/C/04**

This request for expression of interest follows the General Procurement Notice for this Project that appeared in the United Nations Development Business (UNDB) No. WB- P164920 of 14th December 2021

The Government of the United Republic of Tanzania through Tanzania Rural and Urban Roads Agency (TARURA) and Tanzania National Roads Agency (TANROADS) has received a credit from the International Development Association (IDA) towards the cost of Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities (RISE). It is intended that part of the proceeds of the credit will be used to cover eligible payments under the contracts for Consultancy services.

The consulting services ("the Services") intent is to assess and understand compatibility of Agency's software, data capturing, storage and processes under ICT unit and develop Digital Transformation Road Map that will help TARURA on the effective and efficient utilization of human and infrastructure resources, technology and processes to meet its ICT strategic objectives. This ICT assessment assignment is a data-driven evaluation of technology, data capturing, processes and storage, and ICT resources in relation to key Agency goals. The ICT assessment will provide measurable insights and improvements to systematically align information and communication technology to Agency's strategic vision. A comprehensive assessment will measure the health of TARURA's entire ICT environment and will provide an actionable ICT roadmap for the staff, infrastructure, processes, and technology assets to fulfil the Agency's mission.

The total duration for the entire assignment shall be about **Eight 8 calendar months** from contract effective date.

The detailed Terms of Reference (TOR) is attached to this request for Expression of Interest and is also available at TARURA's website **www.tarura.go.tz.** and TARURA RISE Project's website **https://rise.tarura.go.tz** All requests for clarification should be sent through office email **pmurise@tarura.go.tz** and the Client will respond to the requested clarifications. The Consultants would be responsible for ensuring that any addenda available on the website is also downloaded and incorporated.

The Chief Executive TARURA, now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the above services. Interested consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services. The shortlisting criteria are:

A. Core business and 10 years in business.
B. Relevant similar experience, which should specifically include the below:

i) Experience of at least two (2) similar assignments completed in the past 5 years. Information to be provided should include name of assignment, name and full contact address of the client, contract value (in equivalent US dollars) and period (dates) of execution of assignment and the role played in the assignment (Lead or JV partner)
ii) Demonstration of experience of work in similar conditions.

C. Technical and Managerial Capability of the firm (Provide only the structure of the organization, general qualifications and number of key staff). Do not provide CV of the staff. Experts will not be evaluated at the shortlisting stage).

The attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" Fourth Edition, November 2020 ("Procurement Regulations"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

Consultants may associate with other firms to enhance their qualifications but should indicate clearly whether the association is in the form of a joint venture and/or a sub-consultancy. In the case of a joint venture, all the partners in the joint venture shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected. Therefore, each member of JV shall independently meet the requirements of the evaluation criteria. The experience, technical & managerial capability of the Sub-Consultant shall not be evaluated to enhance the qualification of the Lead Firm or JV.

A Consultant will be selected in accordance with the **Quality and Cost Based Selection (QCBS) method** set out in the Procurement Regulations.

Further information can be obtained at the address below during office hours from **08.00 to 17.00 hours** Local time Monday to Friday except public holidays.

Expressions of interest must be delivered in a written form to the address below in person, or by e-mail **pmurise@tarura.go.tz by 25th October, 2023 1430 Hours East African Time**. The firms that will submit their EOI via e-mail must get confirmation of the receipt of their documents. In case the firm does not receive acknowledgement within two days of after sending the documents via email they should call +255752460018/+255759348494/+255622759393 for follow-up.

The address referred above is:

***The Secretary, TARURA HQ Tender Board***
***Street Address: Mtaa wa Kazi 41207 Mtumba,***
***Building: TARURA House***
***Address: P.O. Box 11042, Dodoma, Tanzania.***
***Floor/ Room number: Ground Floor/PMU Office***
***City/Town: Mtumba Government City Area***
***Country: United Republic of Tanzania***
***Telephone: +2557 52460018/+255759348494/+255622759393***
***Electronic mail address: pmurise@tarura.go.tz***

HABARI KITAIFA

# Silaa ageukia upimaji maeneo ya huduma

**Na Munir Shemweta,**
TABORA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kuhakikisha maeneo yote ya huduma za jamii yanapimwa kwa lengo la kuyalinda dhidi ya uvamizi.

Silaa amesema hayo juzi wakati akizungumza na uongozi na watumishi wa sekta ya ardhi mkoa wa Tabora akiwa kwenye ziara ya kufuatilia utekelezaji wa Uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

"Ni vyema wakurugenzi wote wa halmashauri wakapima maeneo yao ya huduma za jamii ili kuyalinda kwa vizazi vya sasa na vile vinavyokuja," alisema.

Alisema kwa sasa ndani ya wizara yake kuna mabadiliko yatakayofanyika katika maeneo yanayoonekana kikwazo kwa sekta hiyo na kutolea mfano wamiliki wa ardhi kuogopa kuchukua hati kwa hofu ya kulipa kodi ya ardhi sambamba na uwezo wa kifedha wa baadhi ya halmashauri katika kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi.

"Kwa hiyo tunaenda kufanya mabadiliko mazuri tunayoamini yakifanyika yatasaidia sekta ya ardhi kuendelea kusaidia sekta zingine kwa kuwa ardhi ni sekta mtambuka" alisema.

Pia aliweka wazi kuhusu usimamizi wa sheria za ardhi akisema halmashauri zimekuwa na msukumo mkubwa kutoka kwa wananchi kuhusu suala hilo na kwamba hakuna msukumo unaosababisha uvunjifu wa amani. Alisisitiza kwamba maeneo ya wazi yabaki kama yalivyo na yale ya huduma kama taasisi yabaki vivyo hivyo pia. 'Tumekubalina maeneo yote ya huduma, shule, vituo vya afya na zahanati yapimwe na yapate hati na mfikishe salama zangu kwa wakurugenzi maeneo yote ya huduma yapimwe na yapate hati.

Waziri Silaa pia alihimiza usimamizi wa sheria katika kutekeleza majukumu sambamba na kuziagiza mamlaka za uhifadhi kuongeza nguvu katika kulinda maeneo hayo ili wananchi wasiyavamie.

"Naamini kabisa maeneo mengi viongozi wanapenda kuhakikisha haki za wananchi zinapatikana na tunapendekeza wanaovunja sheria tunawavunja nguvu wale wananchi kwa kufuata na kuzingatia sheria," alisema Silaa.

Waziri Silaa alihitimisha ziara yake ya siku moja katika mkoa wa Tabora kwa kutembelea ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Chuo cha Ardhi Tabora na kitega uchumi cha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (kushoto), akizungumza na Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Husein Sadick, alipotembelea ofisi ya kamishna wakati wa ziara yake mkoani Tabora juzi. **PICHA: WANMMP**

# Kapinga ahamasisha vijana fursa nishati

**Na Mwandishi Wetu,** MBINGA

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, amewataka Vijana kuchangamkia fursa ya kuomba mikopo ili kuwekeza katika sekta ya Nishati inayotolewa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa nchi nzima.



Kapinga aliyasema hayo juzi wakati wa semina iliyoandaliwa na REA kwa Jumuiya ya Wazazi na Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UCCM) iliyofanyika wilayani, mkoani Ruvuma.

Aliwaambia washiriki wa semina hiyo kuwa fursa ya mikopo hiyo nafuu inalenga ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini na kuwataka vijana hao na wazazi kuomba mikopo hiyo.

Naibu Waziri alisema mkopo huo unaotolewa ni wa Sh. milioni 75 ambazo zinatolewa kwa awamu tatu. Alisema awamu ya kwanza na ya pili kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa kituo na ya tatu ni kwa ajili ya kuagiza mafuta na kuanza biashara. Marejesho ya mkopo huo ni kwa miaka saba.

"Wazazi wangu na vijana wenzangu nimeona nikutane na ninyi hapa ili tuunge mkono ajenda ya Rais (Samia Suluhu Hassan) ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia inayolenga kupunguza matumizi ya kuni na mkaa pamoja na kulinda afya zetu. Kwa kutumia ajenda hii, vijana watatumia fursa zinazopatikana ambazo vijana na wazazi mnaweza kuzitumia," alisema.

Mhandisi Kelvin Tarimo kutoka REA, aliyekuwa akitoa semina kwa wajumbe hao, alisema fursa hiyo ni ya Watanzania wote wanaoishi vijijini.

# Balozi China apewa jukumu mradi Mchuchuma

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imempa Balozi mteule wa Tanzania nchini China, Khamis Musa Omar, jukumu la kutatua changamoto za mradi wa kuzalisha chuma wa Mchuchuma Liganga pamoja na kufufua kiwanda cha nguo cha Urafiki.

Mradi wa Mchuchuma Liganga wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, ulipaswa kutekelezwa na mwekezaji kutoka China lakini ulisimama kutokana na changamoto mbalimbali ambazo serikali imesema imeanza kuzitatua. Hayo yalitokana na mazungumzo kati ya balozi huyo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdalah, walipokutana Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kujadili namna ya kuendelea kuvutia uwekezaji kutoka China.

Dk. Hashil alimweleza balozi huyo kuwa mwekezaji wa mradi wa Mchuchuma Liganga ambaye ni kutoka China alikutana na changamoto mbalimbali ambazo anapaswa kuzifanyia kazi atakapokuwa nchini humo.

Alisema kuna mambo mengi mazuri ambayo serikali ya Tanzania inashirikiana na wawekezaji na wafanyabiashara kutoka China na kwamba ni vyema kutumia vizuri uhusiano mwema wa mataifa hayo mawili kukuza biashara na kuvutia ujenzi wa viwanda.

"Rais Samia amekuamini amekupa nafasi ambayo sisi tunaamini utaimudu. Kule kuna changamoto nyingi ambazo pia tunaamini kwa uwezo mkubwa ulio nao utakwenda kuitatua lakini pale utakapohitaji ushirikiano wa wizara tutakuwa tayari muda wowote," alisema.

Pia alisema serikali itaendelea na jitihada za kukwamua uwekezaji huo na kama itashindikana kabisa mwekezaji wa China kuendelea na uwekezaji wa eneo hilo la Mchuchuma Liganga basi atatafutwa mwekezaji mwingine.

Alisema alimweleza balozi huyo kuhusu mradi mwingine wa Maganga Matitu unaohusu uzalishaji wa chuma ambao unafanywa na mwekezaji kutoka China unaokabiliwa na changamoto tofauti tofauti.

Sambamba na hilo, alimweleza Balozi Khamis umuhimu wa kufufua kiwanda cha kuzalisha nguo cha Urafiki ambacho ni ubia kati ya serikali ya Tanzania na China ambacho kilisimama kutokana na changamoto mbalimbali za uendeshaji.

"Kwenye kiwanda cha Urafiki hatua zimeshaanza kuchukuliwa kujaribu kukifufua. Jambo kubwa na la muhimu ni kwenda kulifanyia kazi na mengine yanayohusu maendeleo ya viwanda na kuvutia uwekezaji kutoka China," alisema

Balozi Khamis alisema Wizara ya Viwanda na Biashara ni nyeti katika mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea na kuahidi kuwa atahakikisha anashirikiana nayo kuvutia uwekezaji zaidi.

"Sote tunafahamu kwamba viwanda ni muhimu sana katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Dira ya Maendeleo ya 2020-2025 kwa hiyo lazima tufanye jitihada kuvutia uwekezaji kwenye viwanda," alisema

Alisema wawekezaji kutoka China ni muhimu katika uwekezaji kwenye sekta ya viwanda na aliahidi kuwa atajitahidi kutatua changamoto ambazo wafanyabiashara wa nchi hiyo wamekuwa wakilalamikia.



## Wanawake wapewa siri ya kujiimarisha kiuchumi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAWAKE wameshauriwa kuondoa mfumo tegemezi unaowarudisha nyuma kimaendeleo, badala yake wajenge tabia ya uthubutu, utakaosaidia kuwaimarisha kiuchumi ndani ya familia zao na taifa kwa ujumla.

Hayo yamesemwa jana na Mkuu wa Wilaya Mstaafu, Beth Mkwasa, wakati alipokuwa kwenye maadhimisho ya kila mwezi ya kusemezana kwa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) wa Jimbo Kuu Katoliki Arusha, katika Parokia ya Moyo Safi wa Bikra Maria, Ungalimited jijini Arusha.

Mkwasa ambaye kwa sasa ni mfanyabiashara na mwandishi wa habari mwandamizi mstaafu, alisema Tanzania imejaliwa kuwa na wanawake wengi wenye nguvu na taifa linawategemea, lakini wengi wao bado wanaishi kwa mfumo wa utegemezi.

Alisema kinamama vizuri sasa wajitambue na kuachana na mfumo wa kiafrika wa utegemezi na kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha biashara ndogo.

"Kinamama vizuri sasa mkaachana na utegemezi wa wanaume, sababu wengi wanaofanya hivi mwisho wa siku maisha yao yanaishia pabaya na kushindwa kulea familia hasa pale baba anapoyumba kimaisha au anapofariki,"alisema.

Awali Paroko wa Parokia ya Moyo Safi wa Bikra Maria, Padri Festus Mangwangi alisema WAWATA wamekuwa na desturi ya kusemezana, ili kukumbushana wajibu katika kutekeleza majukumu yao na kujiweka kando na mambo yasiyompendeza Mungu.

Aidha, aliwahimiza watu kupenda kwenda kwenye nyumba za ibada, ili kufafanuliwa neno la Mungu na jijsi gani ya kuishi ili mioyo yao iwe na hofu na Mungu.

Hivyo, aliwataka wanawake katika kusemezana kwao wahakikishe wanawajibika ipasavyo katika kulea familia na kutunza ndoa zao, wazingatie maagano ya ndoa na kuepuka michepuko na mambo yasiofaa kwenye ndoa.

"Leo Dekania ya WAWATA Jiji Mashariki yenye parokia 11 na vigango vyake, wamekusanyika katika Parokia ya Moyo Safi Ungalimited, kwa ajili ya kusemezana na walichagua mada isemayo mama Mkatoliki na imani katoliki, kuitunza, kuitetea na kuisambaza, "alisema.

Alisema mwanamke anawajibu wa kushiriki maendeleo na kuhudumia familia kama shamba la mzabibu pasipo kumtegemea mwanaume.

Padri Mangwangi alisema kila mwanamke anawajibu wa kushiriki shughuli za kiuchumi na kuondoa mfumo wa kiafrika wa kumtegemea mwanaume akafanye kazi.

Mwenyekiti wa WAWATA jimbo hilo, Bakhita Manga, alisema utaratibu wa kusemezana kwa kinamama Wakatoliki, kumesaidia kujenga utume wa kujitolea, malezi, kujitambua na kufundishana. Alisema: "Utaratibu huu wa kusemezana kumesaidia kuwajenga kiimani na mwanamke kutambua wajibu wake na namna ya kushiriki katika maendeleo ya kifamilia na taifa.

# 'Speed' ya unywaji kahawa nchini yaongezeka, yafikia asilimia saba

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KIWANGO cha unywaji wa kahawa nchini kimeongezeka kutoka asilimia tano hadi kufikia asilimia saba, huku serikali ikiweka wazi mkakati wake ni kupandisha zaidi kiwango hicho mpaka asilimia 15, ifikapo mwaka 2025/2026.

Aidha, wastani wa uzalishaji wa zao hilo la kimkakati nchini, kwa sasa umepanda kutoka tani 50,000 hadi kufikia tani 82,000 mwaka huu.

Akizungumza jana kuhusu kukamilika kwa maandalizi ya 'Tamasha la Kahawa Festival 2023' litakalofanyika Oktoba 27 hadi 29 katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Nchini, Primus Kimario, alisema ili kuvutia kasi ya unywaji na uzalishaji wa kahawa, mkakati wa serikali ni kuchochea uzalishaji kufikia tani 300,000 kwa mwaka.

"Jambo lingine, tumeweka mkakati wa kuongeza pato la mkulima. Kipato hicho kitatokana na kuongeza miti ya kahawa na vilevile kuongeza ubora wa kahawa yetu.

"Tuna mkakati sasa hivi kama serikali kuzalisha miche 20,000 kila mwaka na hii itasaidia kuongeza uzalishaji wetu kufikia tani 300,000.

...Zao letu hili pendwa linalimwa katika mikoa 17 hivi sasa. Mikoa ambayo imechukua fursa hii kwa kiwango kikubwa sana ni Katavi, ambao huko nyuma walikuwa hawalimi kahawa. Tuna Mkoa wa Kigoma, tuna Mkoa wa Njombe hasa Wilaya za Ludewa na Makete na tuna Mkoa wa Mara."

Katika taarifa yake, Kimario, ameeleza furaha yake kwamba, Watanzania wasishangae siku si nyingi mikoa ambayo itaongoza kilimo hicho, ikawa ni mikoa hiyo iliyoibukia kwenye kahawa.

Kuhusu tamasha hilo la Kahawa Festival, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa, safari hii wamewaita madaktari nguli nchini, kwa ajili ya kutoa elimu na kueleza faida na manufaa ya unywaji kahawa.

"Kumekuwa na dhana potofu kwamba kahawa inasababisha baadhi ya magonjwa. Kwa hiyo tunavyoleta madaktari ni fursa pia kuuliza maswali na kupima afya zao bure na watapata semina mbalimbali kuhusu kiburudisho cha kahawa,"alisisitiza Kimario.

Maonyesho hayo yanajumuisha wadau wote katika sekta ya kahawa nchini. Pamoja na mambo mengine yatatanguliwa na mashindano ya utayarishaji wa kahawa.



Askofu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Dk. Msafiri Joseph Mbilu (kulia), akimsimika rasmi Katibu Mkuu mpya wa Dayosisi hiyo, Mwalimu Julius Madiga, wakati wa ibada iliyofanyika Usharika wa Handeni, Jimbo la Magharibi, mkoani Tanga Jumapili. Ibada hiyo iliambatana na uzinduzi wa jimbo hilo na kusimikwa kwa Mkuu wa Jimbo, Mch. Ishmael Reuben Ngoda. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mbunge aipongeza serikali kutoa mabilioni jimboni kwake

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MBUNGE wa Kiteto, mkoani Manyara, Edward Ole Lekaita, ameishukuru serikali kwa kuwapatia fedha nyingi na kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ole Lekaita, aliyasema hayo jana, alipopewa nafasi ya kuzungumza wakati wa Mwenge wa Uhuru ulipopita kukagua, kuzindua, kutembelea na kuweka jiwe la msingi, kwenye miradi ya maendeleo mbalimbali yenye thamani ya Sh. bilioni 2.4.

Miradi iliyotembelewa na Mwenge wa Uhuru mwaka huu Kiteto ni uzinduzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya walimu wa Shule ya Msingi Esukuta na Daraja la Orkine.

Pia Mwenge huo ulifungua Shule mpya ya Msingi ya Azimio na kupanda miti 500 na kuzindua na utunzaji wa mazingira katika Shule ya Sekondari Nasa Matui na kuzindua klabu ya wapinga rushwa.

Vile vile, uliweka jiwe la msingi ujenzi wa majengo matatu Hospitali ya Wilaya ya Kiteto na kuzindua mradi wa maji wa RUWASA majengo mapya Kata ya Kaloleni.

Aidha, Ole Lekaita, alisema kupitia miradi mbalimbali iliyotembelewa na Mwenge Kiteto na mingine iliyopo wilayani humo, ambayo haijapitiwa na Mwenge, wamepiga hatua kubwa ya maendeleo.

"Kwa niaba ya watu wa Jimbo la Kiteto tunaipongeza serikali kwa kutupatia fedha za maendeleo, zilizofanikisha miradi ya sekta ya elimu, afya, maji, miundombinu na mengine," alisema Ole Lekaita.

Hata hivyo, alisema wakazi wa Kiteto hawana cha kuilipa, ila wanaiombea ili izidi kushinda Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2023, Abdalah Shaibu Kaim, alimpongeza mbunge wa Kiteto kwa kushiriki kwenye shughuli za Mwenge ulipokuwa Kiteto.

Alisema: "Mheshimiwa Mbunge Ole Lekaita nakupongeza sana kwa kushiriki ipasavyo kwenye mbio za Mwenge kwa mwaka huu, wewe ni mzalendo mtu bingwa kabisa kwani umeonyesha ushirikiano mkubwa na viongozi wenzake wa Kiteto".



Wakazi wa Kijiji cha Gomora, Kata ya Musanja, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakichimba msingi kwa ajili ya kujenga madarasa ya shule shikizi hivi karibuni, ili kuwapunguzia watoto wadogo kutembea umbali mrefu kufuata elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgawo wa umeme wang'ata hadi migodini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika mgodi wa Mwime Two uliopo Kata ya Zongomela Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wamesema kukatika kwa umeme kumekuwa kukiwakwamisha katika shughuli ya uchimbaji wa madini pamoja na kuikosesha mapato serikali.

Shughuli katika mgodi huo zinaelezwa kutumia nishati ya umeme wakati wote hususani katika kuvuta na kuondoa maji ndani ya mashimo, kwamba kukosekana kwa huduma hiyo kunasababisha wachimbaji kushindwa kuendelea na shughuli zao.

Ofisa Uhusiano wa mgodi huo, Christopher Bundala, aliyabainisha hayo jana wakati akiwasilisha kero mbalimbali zinazoukabili mgodi huo mbele ya viongozi wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu Kahama (SHIHABI) waliofanya ziara ili kuona shughuli za uchimbaji zinazofanyika kwa kuzingatia hazi za binadamu.

Alisema mgawo wa umeme unaoendelea hivi sasa maeneo mbalimbali hapa nchini unasababisha wao kushindwa kuendelea na shughuli ya uchimbaji wa madini baada ya mashimo yenye madini kuanza kujaa maji.

Alisema hata hivyo wakati mwingine wanalazimika kutumia gharama kubwa katika kufanikisha shughuli hizo wakitumia jenereta ambapo gharama za uendeshaji wake ziko juu kutokana na gharama za mafuta kuwa juu.

Naye Mihayo Samweli alisema wameanza kutumia mfumo wa uendeshaji wa uchimbaji wa madini wa zamani wa kutumia magenereta kwa ajili ya kuvuta maji shimoni pamoja na kuingiza hewa ndani yake.

Alisema kutumia mfumo huo ni gharama hususani ununuzi wa mafuta ambako pia yamepanda bei zaidi.

Mwenyekiti wa SHIHABI, Solomoni Juma, aliwataka wachimbaji hao kuwa wavumilivu wakati TANESCO linaendelea kulifanyia kazi suala hilo hasa baada ya kupewa miezi sita na Rais Samia Suluhu Hassan, kwamba serikali inatambua mchango wa wachimbaji wadogo katika kuchangia pato la taifa.

Hata hivyo aliwapongeza kwa kufanyakazi kwa kufuata misingi ya haki za binadamu, hakuna ajira za watoto zinazofanyika ndani ya mgodi pamoja na kuwazuia wanawake wachimbaji kuendelea na uchimbaji kwa imani potofu kuwa wakiingia shimo madini yanaondoka.

# Ufichaji taarifa za ukatili wamshtua M/kiti UWT

**Na Resetuta Damian,** BUKOBA

MWENYETIKI wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UWT), Mary Chatanda, ameshtushwa na tabia ya kufichwa kwa taarifa za ukatili mkoani Kagera pamoja na kutowaripoti wahalifu, hali inayofanya vitendo hivyo kuendelea kushamiri katika jamii.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Mji wa Bukoba baada ya kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyojengwa na inayoendelea kujengwa kwenye halmashauri hiyo.

Chatanda alisema kuwa yamekuwapo matukio ya watoto kufanyiwa vitendo vya ubakaji na ulawiti unaofanywa na ndugu wa karibu wakiwamo wazazi wao pasipo kujali madhara gani yanayotokea dhidi yao, kwamba taarifa zimekuwa hazipelekwi kwenye vyombo vya sheria.

Alisema: "Hali imekuwa mbaya ukifika polisi kuulizia taarifa zilizoripotiwa katika madawati ya jinsia unapewa taarifa ya mwezi mmoja pekee watoto jinsi ya kike waliobakwa ni 15 na walio najisiwa ni 25, wahusika wa vitendo hivyo wanatajwa kuwa ni wageni wanaofika katika familia husika. Hatuwezi kufika tusipoweka nguvu," alisema Chatanda.

Kadhalika, aliwatahadharisha wanafamilia kuwa makini na ndugu wanaofika kuwatembelea kuwa wasiwaruhusu kulala nyumbani wakati mwingine wasilale na watoto.

Alisema endapo kutakuwa na wahalifu wa namna hiyo wahakikishe wanatoa taarifa katika vyombo vya sheria bila kujali undugu wao kwani tabia hizo zimekuwa za mazoea katika jamii.

Chatanda alisema: "Tumeamka sisi wanawake kutembea nchi nzima kuelezana jambo hili. Haiwezekani watoto wetu kuendelea kuumia na wengi hawapo katika hali nzuri, tujaribu kutazamana katika mitaa yetu, kwani wako ambao wanafanya na wametulia, wafichueni."

Aidha, alisema wababakaji na walawiti huwa wanatoa vitisho kwa watoto hao kwamba wakisema kwa wazazi wao watawachinja.

Alisema hatua hiyo inasababisha madhara kwenye mwili wa mtoto, hivyo kuwataka wazazi kuwa na utaratibu wa kuwakagua watoto mara kwa mara.

## DC Urambo aapishwa, ataja vipaumbele

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Wilaya ya Urambo mkoani Tabora, Elibarikii Bajuta, ameahidi kusimamia shughuli mbalimbali za kimaendeleo pamoja na miradi ya kimkakati iliyopo wilayani hapa inayogharimu zaidi ya Sh. bilioni 76.

Alitoa ahadi hiyo juzi mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batrida Buriani, baada ya kuapishwa katika hafla iliyofanyika mkoani hapa baada ya mabadiliko madogo ya wakuu wa wilaya yaliyofanywa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan.

Bajuta alisema wananchi wa Wilaya ya Urambo wategemee miradi hiyo iliyopo itamalizika kwa wakati na kuhakikisha anawasimamia makandarasi wote ambao wapo kwenye miradi hiyo.

Awali akizungumza baada ya kumwapisha, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Buriani, alisema kuwa miradi hiyo ya maendeleo isimamiwe kikamilifu ili wananchi waanze kuhudumiwa na kunufaika na miradi hiyo.

Alisema kati ya miradi hiyo upo ujenzi wa bwawa la maji katika Kijiji cha Kalemela 'A' ulioghalimu Sh.bilioni 5.9 iliyoelekezwa wilayani humo kutokana na kuwa na asilimia 32 ya upatikanaji wa maji mkoani hapa.

Alisema ujenzi wa bwawa hilo litawasaidia wananchi wengi na litapunguza adha ya maji katika Wilaya ya Urambo, hivyo alimtaka asimamie vizuri kwa wakati ili wananchi wanufaike.

Alibainisha miradi mingine ambayo ni ujenzi wa kituo cha kupoza umeme unaendelea katika eneo la Uhuru ambacho wanategemea, kwamba pindi utakapomalizika umeme utaunganishwa hadi mkoani Kigoma.

Aidha, alisema kwamba mradi mwingine wa hospitali mpya kongwe ya Wilaya ya Urambo ambapo Rais Samia aliona ni bora kuiongeza na kuifanya kuwa ya kisasa.

Katika hatua nyingine Balozi Burian alimtaka mkuu huyo wa wilaya kuhakikisha anajenga uhusiano na vijana, wananchi kwa kuweka mikutano ya hadhara ili kusikiliza kero zao na kuzitatua kwa haraka.



Ukurasa 12

**Kuondoa katazo mikutano wanasiasa, wasifurahie haki hata kuvuka mipaka**



Ukurasa 13

Sura halisi ya Chongolo alipojitwisha ilani inayomtetea Samia mkoani Katavi


siasa

JUMATANO OKTOBA 11, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**Kilivyo kitendawili mwelekeo mpya wa mamluki Wagner**

# Wanahabari wa leo wanavyotishiwa na maslahi duni, kukosa usalama

**Na Mwandishi Wetu**




USALAMA wa waandishi wa habari ni muhimu katika kutekeleza majukumu ya kupasha umma habari kwa kuhakikisha kuwa kuna uwajibikaji katika kila linalofanyika ili wananchi wanufaike na rasilimali zao, haki itamalaki na demokrasia kushamiri ndani ya taifa.

Kwa wanahabari usalama huanzia kwenye uhuru na ubora wa kipato, hali kisaikolojia, kidijitali, sehemu ya kazi kuwa na vifaa vya kisasa,haki za kisheria kama likizo, stahiki mbalimbali kama posho na kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, matibabu na kulindwa akitekeleza majukumu yake kwenye jamii kama kwenye mikutano ya hadhara.

Pia, haki ya kupata taarifa kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Haki ya Taarifa 2016, ambayo inawataka maofisa wa serikali kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria, ili kusiwe na kikwazo chochote kwa mwandishi wa habari kutekeleza majukumu yake.

Sheria ya Huduma ya Habari mwaka 2016, imeweka kipengele cha kuwabana waajiri kuhakikisha wanahabari wanakuwa na bima za afya, ingawa utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua.

Mwaka jana, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), linachapisha ripoti inayoonyesha ongezeko la asilimia 50 la mauaji ya wanahabari mwaka 2022, ikimaanisha kuwa mwandishi mmoja anauawa kila baada ya siku nne.

Aidha, ripoti hiyo inabainisha kuwa hakuna yeyote aliyekamatwa wala kufikishwa mahakamani katika asilimia 86 ya kesi zilizofunguliwa kwenye mataifa mbalimbali duniani, huku Mexico ikitajwa kuwa kinara kwa mauaji ya wanahabari sawa na Haiti, huku sababu kubwa ikiwa ni kutokana na uandishi wa taarifa za uhalifu, mizozo, rushwa na mazingira.

Ripoti ya 21 ya Waandishi Wasio na Mipaka (RSF) ya mwaka 2023, inayoangazia siasa, jamii na tekonolojia katika mataifa 180 imebainisha kuwa hali ni mbaya katika mataifa 31, ni ngumu kwenye nchi 42, ni tatizo ndani ya nyingine 55 na ya kuridhisha katika nchi 52.

"Kwa maneno mengine mazingira ya uandishi wa habari ni mabaya katika nchi saba kati ya 10, ya kuridhisha kwenye mataifa matatu pekee kati ya 10,"inasema ripoti hiyo.Kielelezo cha Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani kinaonyesha hali tete, kukiwa na kupanda na kushuka kwa kiwango kikubwa na mabadiliko ambayo hayajawahi kushuhudiwa, kama vile Brazili kwa nafasi ya 18 na kuanguka kwa Senegali kwa nafasi ya 31."

"Kukosekana kwa utulivu huku ni matokeo ya kuongezeka kwa uchokozi kwa upande wa mamlaka katika nchi nyingi na kuongezeka kwa chuki dhidi ya wanahabari kwenye mitandao ya kijamii na katika ulimwengu wa kimwili.Kuyumba huko ni matokeo ya ukuaji wa tasnia ya maudhui ya kughushi ambayo huzalishwa na kusambaza taarifa potofu na kutoa zana za kuzitengeneza,"anasema Katibu Mkuu wa RSF, Christophe Deloire

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Tanzania imeshika nafasi ya 143 ikichukua alama 44.02 ikilinganishwa na nafasi ya 123 mwaka 2022 ikiwa na pointi 48.28, katika moja ya mambo muhimu ambayo ripoti hiyo imeangazia kwa taifa hili ni maslahi duni hali inayowafanya washindwe kuwa huru katika kutekeleza majukumu yao.

"Waandishi wanalipwa malipo duni huku kazi yao ikiwa ni ya hatari. Serikali inawajibu mkubwa kwenye uchumi wa vyombo vya habari, vyombo vya binafsi vinapata matangazo yake kati ya asilimia 40 hadi 80 kutoka serikalini, na Februari mwaka 2022 serikali iliahidi kutoa matangazo kwa vyombo vyote kwa ushindani,"inasema sehemu ya ripoti hiyo.

Kuhusu usalama RSF inasema mwaka 2022 vyombo na waandishi wa habari waliacha kukosoa utawala kwa kuhofia kufungiwa, kushikiliwa na kutekwa huku serikali ikieleza kwamba hakuna jambo kuhusu Azory Ngwanda aliyetoweka katika mazingira tatanishi mwaka 2017.

Ofisa Programu anayeshughulikia utafiti, mafunzo na machapisho wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Victor Maleko, anasema kuna mabadiliko makubwa kwa madhila wanayopitia waandishi wa habari kutokana na ushirikiano uliopo baina ya wadau wa habari na serikali.

Anasema mwaka jana yaliripotiwa madhila 26 lakini kwa mwaka huu yamerekodiwa tisa pekee, na kwamba mengi ni mvutano baina ya mamlaka na wanahabari kukamatwa na vitisho.

"Madhila wanayokutana nayo zaidi ni kutishiwa maisha na kukamatwa na polisi, mfano mwaka jana wengi walikamatwa na kutishiwa wakiambia usiandike habari hii nitakuondoa kwenye hili eneo au nitakukamata. Mambo yanayofanywa na taasisi za serikali kama wakuu wa wilaya au makatibu tawala, lakini kutumia mazungumzo kumesaidia,"anasema Maleko.

Aidha, kuna nyakati ambazo waandishi hukosea na kwenda kinyume na sheria na taratibu na wanapoambiwa huwa wabishi kwamba wako kwenye utekelezaji wa majukumu yao, anaeleza na kuongeza: "Baadhi ya maeneo tumeona wenyewe wanakuwa chanzo cha migogoro, anaambiwa usifike hapa anafika kwasababu tu ni mwandishi, kuna baadhi wanakosa weledi au kutojua, kuna wengine wanaandika mambo yanayoleta taharuki kwenye nchi au eneo jambo ambalo siyo sawa."

Aidha, anashauri kila mmoja, waandishi na serikali wafanyekazi kwa kuzingatia maadili ili kuondoa mvutano na kwamba kila upande ukisimama eneo lake na kuzingatia misingi haitafika kwenye hatua ya kupishana, kwa mujibu wa Maleko, na kuona umuhimu wa kuzijua sheria na taratibu zilizopo kwa kuwa hakuna taaluma iliyo juu ya sheria.

Kuhusu malipo na usalama wa wanabahari, anasema ili mwandishi atekeleze majukumu yake vizuri ni muhimu akalipwaipasavyo ikiwa ni pamoja na kuwa na bima ya afya ili afanyekazi kwa kujiamini.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari (JOWUTA), Mussa Juma, anasema usalama wa waandishi ni mdogo kutokana na kwamba wengi hawana kipato cha uhakika huku mikoani zaidi ya asilimia 95 hawana ajira wala mikataba.

"Serikali isimamie sheria ili wawe na maslahi bora na usalama iwe ni sehemu ya masuala ya msingi ya sheria za wanahabari nchini. JOWUTA tunafanya mafunzo ya ulinzi na usalama kazini, pia tunakusanya taarifa za waajiriwa na wasio na ajara, ili tuishawishi serikali kulipa madeni ya vyombo vya habari ili viwalipe wafanyakazi,"anasema.



Baadhi ya wananchi wakifuatilia mikutano ya kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

# Kuondoa katazo mikutano wanasiasa, wasifurahie haki hata kuvuka mipaka

**Na Reubeni Lumbagala,**

DODOMA

BINADAMU anazo haki nyingi zinazogusa nyanja zote za maisha yake, zipo haki zinazoangazia masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira. Na katika kuhakikisha kuwa hakuna anayepunjwa haki zake , katiba imeziainisha na kuziandika kwenye ibara inayozitaja haki za binadamu ikiwapo ya msingi kuwa kila mtu anayo haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa utu wake tena anayo haki ya kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka serikalini na jamii kwa mujibu wa sheria .

Siasa ambayo ni nyanja kubwa kwenye jamii inayoweza kuonekana karibu kila sekta na tasnia, wanasiasa wanayo haki ya kuunda vyama, kuwa wanachama wake, kufanya mikutano ya hadhara, kutangaza sera, ilani na mipango yao katika majukwaa yao.

Yote hayo yanalenga kutafuta kuungwa mkono kutoka kwa wananchi na hata washirika nje na ndani ya nchi.

Hata hivyo, haki hizo na za binadamu zina mipaka yake, ambayo ni ile hali ya kufurahia haki yake bila kumsababishia mwingine maumivu au kuvuruga haki za wengine.

Kwa yeyote anayetumia haki yake ni vyema kuzingatia kuwa anapofurahia, havunji haki na stahili za watu wengine ili kuendelea kujenga jamii inayoheshimu haki na utu wa binadamu na wa Watanzania wote.

Leo vyama vya siasa vinasherehekea kuondolewa zuio la kutofanya mikutano ya hadhara kwa takribani miaka sita.

Havitaisahau Januari 3, 2023 Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa ikulu Dar es Salaam, anatangaza jambo jema akisema :"Uwepo wangu leo mbele yenu ni kuja kufanya ruhusa, kuja kutangaza lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara, sasa limeondoka".

> Kajijengeni kwa wananchi, elezeni mmejipanga vipi ili warudi wawaunge tena mkono tukienda kwenye uchaguzi vyama vikasimame, hilo ndilo la kufanya.

Kutokana na kudumisha demokrasia na kusimamia maridhiano na uhimilivu wa kisiasa Rais Samia aliondoa zuio hilo na kutoa fursa kwa vyama vya siasa kufanya mikutano na kujijenga, ikizingatiwa kuwa mwaka 2024 kutafanyika uchaguzi wa serikali za mitaa, utakaofutiwa na mkuu 2025.

Rais Samia akifungua mkutano wa Baraza Maalum la Vyama vya Siasa kutathmini utekelezaji wa mapendekezo ya Kikosi Kazi uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Kulius Nyerere (JNICC), anatoa rai kwa wanasiasa kutumia vyema uhuru wa kutoa maoni kupitia mikutano ya hadhara kuchambua hoja na fikra zenye tija zinazolenga kuimarisha utendaji serikalini badala ya kutumia majukwaa kudhalilisha watu wengine, kuibua hisia za kidini, ukabila au kubaguana.

"Tumeruhusu mikutano ya hadhara tukiwa na nia vyama vya siasa vizungumze, wananchi wasikie sera zao, mada zao, mipango yao ili vyama vikue na virudishe wale waliowapoteza, na ndiyo maana ya kutoa fursa hii ya mikutano ya hadhara, si watu wasimame kutukana, kukashifu, kuchambua dini za watu lakini sishangai kwanini haya yanatokea kwa sababu ya kuzungumzwa hakuna" anasema Rais Samia.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye tamaduni na mila nzuri za kujivunia kwa mataifa mengine. Si mila wala desturi za kutukana, kukashifu, kubagua wengine kwa sababu zozote zile. Hivyo, ni vyema wanasiasa kupima na kuzingatia mijadala isiyoibua mitafaruku ili kujenga umoja na mshikamano nchini.

Ni jambo baya kutaka kujijenga kisiasa kwa kuchafua wengine, unaweza kuchukuliwa kama uvunjifu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi, lakini pia kwa upande mwingine ikaonekana kama mwanasiasa anaonewa lakini pengine hakuna mwenye nia ya kumsumbua mwingine katika hatua za kujenga taifa lenye uhuru wa kisiasa na linathamini uwepo wa vyama vingi.

Yapo mambo mengi ambayo wananchi wanapenda kusikia kutoka kwa viongozi na wanasiasa kupitia mikutano ya hadhara, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Wanasiasa watawakosea heshima wapigakura wao na wapenzi wa vyama vyao walioamua kutoa muda wao kwenda kusikiliza hoja na sera mbalimbali katika mikutano ya hadhara halafu wakutane na lugha za matusi, kebehi na udhalilishaji dhidi ya watu wengine.

Pamoja na tofauti za kisiasa na kiitikadi walizonazo wanasiasa, lakini tofauti hizo hazipaswi kuwa sababu ya kudhalilishana katika majukwaa ya hadhara badala yake nguvu ya hoja iwe msingi wa kuchambua masuala mbalimbali ya kitaifa.

Pia, ni vizuri kwa wanasiasa kutambua kuwa wananchi wanao uwezo mkubwa wa kuchambua hoja, kufuatilia na hivyo kutumia majukwaa ya kisiasa kuleta upotoshaji na taharuki ndani ya jamii.

Kutusi kukebehi kunaweza kuonekana kama jambo ambalo linalochafua vyama vyao na hivyo kuwa katika hatari ya kukosa uungwaji mkono kwa wananchi na hatimaye kushindwa katika chaguzi zijazo.

Wananchi wanakabiliwa na kero mbalimbali katika maeneo yao, wanataka kusikia viongozi walivyojipanga kutatua kero hizo kwa ustawi bora wa maisha yao.

Wanasiasa kuacha kuongelea masuala yanayogusa maisha ya wananchi na kutafuta utatuzi wa kero zao, ni kukosa uhalali wa kuaminika kwa wapigakura na hivyo kukosa uungwaji mkono na wananchi.

Katika mkutano huo Rais Samia anasisitiza, "kajijengeni kwa wananchi, elezeni mmejipanga vipi ili warudi wawaunge tena mkono tukienda kwenye uchaguzi vyama vikasimame, hilo ndilo la kufanya."

Siasa safi zitaendeleza tunu ya amani tuliyonayo sasa. Undugu, mshikamano na umoja wa kitaifa utaendelea kudumu endapo wanasiasa wataheshimiana huku lugha za kistaarabu zikizingatiwa katika uzungumzaji kwenye majukwaa ya kisiasa.

Itoshe wanaseiasa kuona kuwa, Rais Samia ametoa darasa muhimu kwa umma kuhusu kujenga hoja kwenye mikutano ya hadhara na kuachana na lugha za matusi.

Yapo mambo mengi muhimu ya kuongea kwa wananchi majukwaani, ila endapo mwanasiasa atakosa la kuzungumza, busara imtume kunyamaza awaachie wengine wenye hoja kuongea ili serikali izifanyie kazi hoja zinazoibuliwa katika mikutano ya hadhara kwa manufaa ya raia na kuongeza kasi ya maendeleo.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Sekondari Mlali Dodoma. Maoni: 0620 800 462.***

# Sura halisi ya Chongolo alipojitwisha ilani inayomtetea Rais mkoani Katavi

## • Kilio cha umma, mawaziri 'kizimbani' kujibu

**Na Neema Hussein,** MPANDA

LEO inapotajwa jina Daniel Chongolo, ni kubwa kitaifa, maana ndiye anashika usukani wa utendaji kuhakikisha kilichonadiwa na CCM, kwenye uchaguzi uliopita kinatekelezwa.

Jana Chongolo huyo alikuwa Mkuu wa Wilaya na juzi akihudumia katika ofisi ndogo ya makao makuu ya CCM, huku kabla ya hapo alikuwa mwanahabari kazini.

Wakati anateuliwa kushika nafasi ya sasa, kama ilivyo kawaida ya jukumu kubwa hasa la kisiasa, kukawapo minong'ono na maswali hasa mitandaoni 'ataweza kweli?' maana CCM ni 'ngome kubwa na ngumu'.

Kihistoria, nafasi hiyo imeshuhudiwa kutumikiwa na magwiji kina: Pius Msekwa, muasisi wa uhuru Rashid Kawawa, Horace Kolimba, Lawrence Gama, Yusuph Makamba, Philip Mangula, Wilson Mukama na Abdulrahman Kinana.

Hapo kijana wa unasaba pekee na Chongolo ni Bashiru Ally, ambaye ana faida jina lake lina utangulizi 'Daktari', tena katika fani ya Sayansi ya Siasa, akitokea kushika chaki na kutafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma.

Pengine maswali kwa Chongolo wakati ule, hayakuwa na majibu ya kulikoni Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kamkabidhi dhamana hiyo nzito, kijana mkuu wa wilaya tafsiri ikibaki ni siri ya chama.

Kutimu sasa, Chongolo anahesabu miaka miwili na nusu kazini. Pia, kwa kuwa ni siku tatu zijazo kunatimizwa kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, mtu muhimu katika historia ya CCM, msingi wa majibu uaanzia hapo.

Rafiki yake Nyerere, Rais wa China, Mao Tse Tung, alipenda usemi 'no research no right to speak' kwa maana pasipo utafiti, hakuna haja ya kujenga hoja.

Pia, mdau muasaisi wa harakati za kudai mfumo wa vyama vingi tangu akiwa mwanafunzi wa uhandisi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Joseph Mbatia, anapenda kuliendeleza akinena 'hoja kwa vielelezo'.

Vilevile wanasheria wana kundi mojawapo la uthibitisho, kwa dai lolote linalotolewa ikitamkwa kwa kizungu 'circumstantial evidence', kwa maana ya ushahidi wa mazingira.

Vyote hivyo, ndivyo vinavyotoa majibu sasa, kulikoni Rais Dk. Samia kuangazia jicho kwa Mkuu wa Wilaya Chongolo, kuwa mtendaji wake mkuu wa CCM, inayoielekeza serikali cha kufanya, kulingana na ilani walioinadi, ambayo watakuja kuwajibu Watanzania 2025.

Inajulikana, si kazi nyepesi kubeba dhamana ya kusafisha lawama dhidi ya Rais, mbele ya Watanzania milioni 60.

### DARASA LA KATAVI

Mara baada ya kuingia katika wadhifa wake, Chongolo amedumu na mtindo wa utendaji



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alipokagua miradi, katika ziara yake mkoani Katavi, wiki iliyopita. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

wa kuibua kasoro ndani ya chama, kisha anazikosoa akilenga kutakatisha mfumo na ilani ya CCM, kutekeleza ilichoahidi, ili utakapofika uchaguzi ujao, kwa serikali za mitaa 2024 na mkuu, 2025 kote ziuzike.

Hilo limeshuhudiwa hasa katika harakati za kukemea rushwa katika uchaguzi wa viongozi ndani ya chama, pia dhidi ya 'wanaojipitisha'kuteuliwa wagombea kwa safari ya uchaguzi ujao, serikali ya mtaa mwakani na uchaguzi mkuu 2025, akisema 'marufuku kujipitisha, wakati haujatimu.'

Upande wa serikalini, ana staili aliyobuni kufanya ukaguzi 'mkoa kwa mkoa' kuangalia maendeleo ya utekezaji miradi ya kiserikali, kasoro anazoibua kupata majibu wakati huohuo.

Staili yake ziarani anawawajibisha mawaziri wenye dhamana papo kwa hapo kuyatolea ufafanuzi, kisha 'anagonga 'msumari' wa maelekezo ya chama, akibeba dhamana ya Mwenyekiti, Dk. Samia.

Nipashe iliyokuwa sehemu ya ziara yake ya siku tano mkoani Katavi iliyoisha Jumamosi iliyopita kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM, imenasa ushuhuda wa mambo kadhaa.

Mosi, muda wote anadumu na dhana "Hapa kazi tu!' aliyorithi kutoka kwa John Magufuli akiwa mtendaji wake wilayani, akifanya kazi tangu alfajiri hadi usiku mfululizo.

Pili, lililo tata linaloibuliwa na wananchi, anawaachia majibu, katika sura ya 'serikali kuwawajibikia wananchi kabla hajaondoka mahali hapo, ili 'kazi iendelee!'

Ziara ya wiki iliyopita ilianza pale Oktoba 2, saa 10. jioni, Chongolo alipowasili katika Uwanja wa Ndege Mpanda na kupokewa kwa shangwe na vikundi vya burudani pia ngoma za asili katika uwanja wa ndege wa Mpanda na kuelekea Ofisi za CCM mkoa wa Katavi.

Ilimchukua nusu saa ya faragha na viongozi wa chama chake, kisha akaurejea umma kuwatajia mambo makuu matatu aliyoyafuta kwao Katavi; kukagua miradi ya maendeleo, kuimarisha uhai wa chama; na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020.

Katika hilo la mwisho, akawaorodheshea maudhui ya ahadi kama vile maboresho katika maji, barabara, umeme, kilimo na mifugo, katika kupata uhalisia wake.

Hata hivyo, Chongolo akazungumzia suala la watu wanaojiita 'Kamchape' Katavi wanaojihusisha na ushirikina wakiweka kambi eneo Karema, wilaya Tanganyika, wakidai wanawafichua wachawi.

Hapo anawataka wananchi kuachana kuendekeza mambo yenye taswira za umaskini kwa mkoa wa Katavi, akiwashauri: "Mkoa wa Katavi ni mkubwa, umejenga historia kubwa, hauwezi kuendekeza ushirikina kama daraja la kufanikiwa,"

Ni baada ya kulala Tanganyika alikokagua kituo cha afya Ikola, Bandari ya Karema na kituo cha afya Kagunga, Oktoba 3, pia akafanya mkutano wa hadhara Kasekese na kurejea mjini Mpanda.

Ni msafara usiopoteza muda 'hapa kazi tu' mnamo saa 1:00 asubuhi, safari inaanza Oktoba 4 , akiondoka kuelekea Halmashauri ya Mpimbwe ambako akianza ukaguzi wa Barabara za Usevya, Kibaoni hadi Stalike, zinazojengwa kwa kiwango cha lami.

Ni safari ya ukaguzi 'mbiombio' iliyowafikisha katika Daraja la Msadya na Kavuu, vilevile mradi wa maji Usevya na Majimoto.

Ni baada ya hapo ilikuwa siku ya Oktoba 5, msafara uliolala katika eneo la Majimoto na saa moja asubuhi, uliondoka kuelekea Halmashauri ya Mlele.

> Staili yake ziarani anawawajibisha mawaziri wenye dhamana papo kwa hapo kuyatolea ufafanuzi, kisha 'anagonga 'msumari' wa maelekezo ya chama, akibeba dhamana ya Mwenyekiti, Dk. Samia.

Hiyo ikachukua zaidi ya saa mbili kufika, ambako Katibu Mkuu wa CCM akajikita katika kukagua bwawa la Maji Nsekwa, linalojengwa kutunza na kuhifadhi maji ya mvua, kumaliza changamoto ya maji katika eneo hilo.

Wakati akiendelea kutoa maelekezo katika bwawa hilo, akakutana na wenyeji wake, Chifu wa Kabila la Wakonongo wenye utawala wa eneo la Kalovya. Akasalimiana na Chifu Michael Kayamba, aliyemkaribisha katika halmashauri hiyo.

Baada ya hapo alitembelea na kukagua kituo cha kupozea umeme wa Gridi ya Taifa kilichopo Inyonga, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.

Msafara huo uliokuwa katika ratiba kali uliondoka kuelekea mjini Mpanda, asubuhi ya Oktoba 6, ukielekea katika Halmashauri ya Nsimbo, ambako Chongolo akaanza kwa kukagua Shule ya Sekondari Ugala, Mradi wa Maji Katambike, Skimu ya Umwagiliaji Ugala kisha akazungumza na wananchi.

Msafara ulirejea mijini Mpanda, asubuhi Oktoba 7, alikohitimisha ziara yake katika Manispaa ya Mpanda. Hapo akaanza kwa kuzindua Mradi wa Vibanda vya CCM wilaya ya Mpanda, kisha akatembelea na kukagua Hospitali ya Rufani mkoa wa Katavi, ambayo ni mpya, alikokagua.

Baadaye jioni, akawa na mkutano mkubwa uliofanyika katika viwanja vya shule ya msingi Kashato vilivyopo Manispaa ya Mpanda, ambako akatumia nafasij hiyo kuiwawajibisha mawaziri wenye dhamana kutoa ufafanuzi wa vilio vya umma, walivyovwaibua wananchi.

***• Mwandishi alikuwa sehemu ya ziara. Kesho usikose, hoja zinazotawala kwenye ziara.***

# Kilivyo kitendawili mwelekeo mpya wa mamluki Wagner

**Na Enock Charles**



Mmoja wa kamanda wa Wagner akitoa maelekezo kwa wanajeshi katika moja ya nchi za Afrika

MWEZI umetimia tangu kufariki kwa kiongozi wa kundi la mamluki wa Wagner na mshirika mkubwa wa Rais wa Urusi, Vladmir Putin , marehemu Yevgeny Prighozin, akipoteza maisha mjini Tver kaskazini mwa Moscow kwenye ajali ya ndege.

Anatwaliwa duniani pamoja na abiria saba na mshirika wake wa karibu ambaye pia anaelezwa kuwa alikuwa makamu wake, Dimitry Utkin.

Kampuni yake ya kijeshi imekuwa na majukumu muhimu kuisaidia Moscow katika uvamizi wake wa kijeshi nchini Ukraine tangu Februari mwaka jana. Hata hivyo, siku za mwisho za uhai wake kiongozi huyo alikosoa vikali uongozi wa kijeshi uliopo nchini Urusi akiwemo Waziri wa Ulinzi Sergei Shoigu na Mkuu wa Majeshi, Valery Gerasimov kwa kile alichodai ni uzembe wa kushindwa kusambaza silaha kwa mamluki wake jambo lililosababisha washambuliwe kirahisi na kupoteza pambano vitani.

Kufariki kwa kiongozi huyo kumeeibua tafakuri ya ni upi mwelekeo wa kundi hilo kwa sasa lenye umaarufu mkubwa duniani kutokana na harakati zake katika mataifa mbalimbali. Wagner inafahamika kwa upambanaji wake likiwa vitani kiasi cha kukodishwa kutumika katika nchi kadhaa ikiwamo Syria na baadhi ya mataifa ya Ukanda wa Sahel kama Niger, Chad na Senegal na hata Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR). Hata hivyo kundi hilo limekuwa likilalamikiwa kwa mauaji , ukatili na utesaji.

**UJIO WAKUMRITHI**

Mara baada ya kufariki kiongozi wao, Rais wa Urusi Vladimir Putin, anawataka kula kiapo cha utii kwa rais na wiki iliyopita ameemteua mkuu mpya wa kundi hilo, Andrei Troshev, ambaye ni mmoja wa makamanda wakuu wa zamani wa kundi hilo akimtaka kusimamia wapiganaji wa kujitolea nchini Ukraine.

Kiongozi huyo mpya ameteuliwa wakati Rais Putin akijaribu kujihakikishia mamlaka yake kufuatia maasi ya Wagner ya Juni mwaka huu.

Katika muda wa saa 24 pekee, waliasi na kutuma wanajeshi katika mji wa kusini wa Rostov-on-Don mojawapo ya ngome kuu za kijeshi za Urusi, kisha kuahidi kuelekea Moscow, kabla ya kurudi nyuma.

Kutokana na huduma ya kundi la Wagner Urusi iliweza kudhibiti baadhi ya maeneo Ukraine.Hata hivyo, vikosi vya Urusi havidhibiti kikamilifu majimbo ya Kherson, Zaporizhzhia, Donetsk na Luhansk, na vimelazimika wakati mwingine kusalimisha maeneo kadhaa kufuatia mashambulizi kutoka Ukraine. Makabiliano baina yake na Ukraine yanaendelea kuripotiwa sehemu mbalimbali za nchi hiyo.

Idara ya ulinzi wa anga inasema imeziharibu ndege 11 zisizo na rubani zilizorushwa na Ukraine katika maeneo ya Kursk na katika mkoa wa Kaluga takriban kilomita 200 kusini magharibi mwa Moscow.

Kundi hilo pia linadaiwa limekuwa muhimu katika kueneza ushawishi wa Urusi kupitia kampeni za vyombo vya habari ambazo zinadharau nchi za Magharibi.



Kamanda Mkuu wa Wagner, Andrei Troshev. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Wagner ina ushawishi mkubwa katika bara la Afrika ambapo inatoa usalama kwa baadhi ya viongozi wa Afrika kwa kupatiwa madini na makubaliano mengine ya kimkakati ya kiuchumi na kijeshi, vinadai vyombo vya Magharibi.

Kundi hilo pia limekuwa muhimu katika kueneza ushawishi wa Urusi kupitia kampeni za vyombo vya habari ambazo kimsingi zinadharau Magharibi huku likiendesha operesheni za maelfu ya mamluki wanaofanya kazi Mali, CAR na Libya.

Mapema wiki iliyopita, Russia House, kituo cha kitamaduni chenye uhusiano na Wagner kilichoko katika mji mkuu wa CAR, Bangui, kilitangaza maonyesho ya biashara ya miezi mitatu kwa wafanyabiashara wa Urusi wanaotaka kupanua shughuli katika eneo hilo.

Hii inaweza kuwezesha kampuni zinazohusishwa na Wagner kufanya kazi nchini CAR na kukwepa vikwazo vya Magharibi.

Mamluki wanaofanya kazi nchini CAR wameshutumiwa kwa ukatili wakati wakipigana na waasi nyuma ya nchi hiyo kutokuwa na utulivu.

Serikali ya kijeshi ya Mali pia imekuwa ikiitegemea sana Wagner baada ya kumaliza makubaliano ya usalama na Ufaransa na kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa.

Kundi hilo pia linadaiwa limekuwa muhimu katika kueneza ushawishi wa Urusi kupitia kampeni za vyombo vya habari ambazo zinadharau nchi za Magharibi.

Huko CAR, ambapo vikosi vya Wagner vilialikwa na Rais Faustin-Archange Touadéra mwaka 2018, mamluki hao wameenea katika sekta ya vyombo vya habari, mbao na hata uzalishaji pombe kali ya Vodka ili kuunganisha masilahi ya kiuchumi katika nchi hiyo yenye utajiri wa madini. Baada ya zoezi hilo kufeli la kuongoza uasi, Prigozhin alichapisha video zake za kwanza, akionekana inawezekana ilipigwa barani Afrika - kwenye chaneli za Telegram zinazohusishwa na kundi la Wagner.

Mtu ambaye anaonekana kuwa kiongozi wa mamluki mwenye umri wa miaka 62 yupo kwenye video akiwa amesimama katika jangwa akiwa amejificha na akishikilia bunduki mikononi mwake. Kwa mbali, kuna watu wengi wenye silaha na lori la mizigo.

Anasema Wagner inaendesha shughuli za uchunguzi na utafutaji na kuifanya Urusi kuwa kubwa zaidi katika mabara yote, na Afrika kuwa huru zaidi.

Mustakabali wa Wagner barani Afrika ulikuwa wa shaka hata kabla ya kifo cha Prigozhin.

Vyanzo vilivyo karibu na kundi hilo vinasema kulikuwa na mipango inaendelea, ikiongozwa na Naibu Mkurugenzi wa kitengo cha kijasusi cha kijeshi cha Urusi GRU, kuchukua nafasi ya sehemu kubwa ya Wagner na kundi sambamba la mamluki.

Prigozhin anasemekana kupinga hili kwa hasira na alikimbia kurudi kutoka Mali hadi Urusi ili kujaribu kulizuia.

Kinachoshumbua kichwa Kremlin sasa ni nini cha kufanya na wapiganaji wa Wagner 25,000, waliotawanyika katika nchi kadhaa duniani, ambao wengi wao waliona uaminifu wao kuwa kwa Prigozhin, badala ya wizara ya ulinzi ya Moscow iliyodharauliwa sana. **BBC**



## Vyuo vikuu vyatakiwa kufanya utafiti wa kusaidia jamii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amevitaka vyuo vikuu nchini kufanya utafiti utakaosaidia kutatua kero zilizopo kwenye jamii.

Prof. Mkenda alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wanataaluma wa Chuo Kikuu Huria (OUT).

Alisema utafiti huo ni pamoja na zile zinazochochea ukuaji wa sekta ya kilimo kutokana na Watanzania wengi kujishughulisha na sekta hiyo.

"Changamoto yoyote ni fursa kwa watafiti kuangalia hapa tunaweza kufanya nini ili wananchi wafanye kilimo ambacho kina tija, fanyeni utafiti na kuja na majawabu, utafiti hauwezi ukawa wa kitaifa peke yake, juhudi za utafiti ni za kimataifa," alisema.

Aidha, alisema utafiti utakaofanywa na vyuo hivyo uwe na sifa ya kushindanishwa na zinazofanywa na vyuo vingine duniani.

"Sayansi haina mipaka ya nchi wala dini wala kabila, sayansi ni ile ile, mtu anaweza kuwa Urusi akagundua kitu Marekani atajifunza kwake," alisema.

Alihimiza chuo hicho kujikita katika kutoa mafunzo na kuzalisha wataalamu na sio kukusanya fedha.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Elifas Bisanda, alisema taifa lina uhaba mkubwa wa walimu wa sayansi na hisabati na kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) unaotekelezwa chini ya wizara hiyo, chuo hicho kimeanza ujenzi wa maabara saba za sayansi.

Alisema maabara hizo zitajengwa katika mikoa ya Arusha, Pwani, Dodoma, Mwanza, Mtwara, Kigoma na Njombe.

# Washauri njia kupunguza matukio ya watu kujiua

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KUTOKANA na kuongezeka kwa matukio ya kudhuru wengine na kujidhuru ikiwamo kujiua, serikali imeombwa kuja na mpango mkakati wa kutoa elimu ya kukabiliana na magonjwa ya afya ya akili ili kuondokana na vitendo hivyo.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano, Mchungaji Dk. Elias Silayo, aliyasema hayo kwenye kongamano tiba la kitaifa lililoshirikisha wadau mbalimbali.

Alisema kuna ongezeko la magonjwa hayo na kutolea mfano Hospitali ya Mwanyamala kwa siku inapokea wagonjwa 30.

"Je, hospitali zingine hali ikoje? Na je, wale ambao hawapelekwi hospitali, umefika wakati ambao labda serikali yetu kupitia wizara zake za kisekta wanapaswa kuja na mpango mkakati kwa ajili ya jambo hili la afya ya akili," alisema.

Alisema watu kuuana imekuwa kama jadi kwenye jamii na kutaka kujitathmini.

Mrakibu wa Jeshi la Polisi, ACP Mohamed Haji, alisisitiza kutolewa kwa elimu kwa makundi mbalimbali kuhusu tatizo la afya ya akili.

"Kama akili yako haitakuwa timamu katika kazi zetu sisi kuna changamoto nyingi, aidha utaleta madhara kwa mtu mmoja mmoja au kwa jamii ili tu kuondokana na hayo tunafanya juhudi ya kutoa elimu ya afya ya akili," alisema.

Daktari mbobezi wa masuala ya maendeleo ya binadamu ya afya ya akili kinga, Dk. Myrose Majinge, alisema asilimia zaidi ya 75 ya maradhi yote kwa binadamu yanasababishwa na magonjwa ya afya ya akili ikiwamo chuki.

Alisema: "Mtu anaambiwa samehe anasema 'over my dead body' mimi sisamehi, sasa unapomchukia mtu nani anaathirika nani anaumia".




Mratibu wa maonyesho ya kuku 2023, Sufian Zuberi (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maonyesho hayo yanayotarajiwa kufanyika Oktoba 13 na 14, 2023 Mlimani City. Kushoto ni Vincent Nyingi kutoka Premium Ingredients na (kulia) ni Dk. Kimory Ryoba kutoka Thrishool Exim ambao ni miongoni mwa wadhamini wa maonyesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bil.8/- zatengwa kudhibiti magonjwa ya kupe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh.bilioni nane kwa mwaka 2023/24 za ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa majosho ya kuogeshea mifugo na ununuzi wa dawa ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe, ambayo yanachangia vifo vya mifugo.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Herzon Nonga, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha maofisa wa wizara na Kamati ya Utendaji ya Chama cha Mazingira na Ufugaji Tanzania.

Alisema katika fedha hizo Sh. bilioni 3.8 zinakwenda kununua dawa za kuogesha mifugo na majosho yanayotegemewa kujengwa, yatagharimu Sh.bilioni tano ikiwa ni mkakati wa serikali wa kuhakikisha Tanzania kunakuwa hakuna magonjwa ya wanyama.

Kuhusu migogoro ya ardhi, Prof. Nonga alisema migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi inachangia uvunjifu wa amani.

Alisema: "Ni muda mwafaka wa kuona kwamba kwanini Watanzania tuendelee kuishi maisha ya kugombana, maisha ya uhasama mkulima anamuona mfugaji ni mtu mbaya sana au mfugaji anamwona mkulima ni mtu mbaya sana Watanzania tunapendana tunaishi kwa kuheshimiana".

# Bil.13.6/- kuondoa matumizi ya kuni magerezani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza nchini lipo katika hatua za mwisho za kuachana na matumizi ya kuni kupitia mradi wa nishati safi unaotarajiwa kugharimu Sh.bilioni 13.6.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuzitaka taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100 kuacha kutumia nishati hiyo ili kulinda mazingira.

Kaimu Kamishna wa Utawala na Rasilimali Watu wa Jeshi hilo, DCP Jeremia Katungu, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua kikao cha menejimenti ya jeshi hilo cha kupitia rasimu ya pili ya andiko la mradi huo kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu magerezani mwaka 2023 -2026.

"Nisisitize kuwa huu ni mradi muhimu sana kwani ni maelekezo ya Rais kwa taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100 kuacha kutumia nishati ya kuni ili kulinda mazingira," alisema.

Alibainisha kuwa katika andiko hilo, mradi huo unatarajia kugharimu Sh. bilioni 13.6 kwa kipindi cha miaka 2023 hadi 2026, huku Sh. bilioni 1.2 zikiwa tayari zimetengwa na serikali kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake kwa mwaka 2023/24.

"Gharama za utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka 2024/25 zinakadiriwa kuwa Sh.bilioni 7.02 huku gharama kwa mwaka 2025/26 zikiwa Sh.bilioni 5.4," alisema.

Alisema nishati zinazotarajiwa kutumika katika mradi huo na ambazo tayari baadhi yake zilishaanza kutumika katika baadhi ya magereza ni gesi vunde, gesi ya mafuta ya petroli, gesi asili na mkaa mbadala.

"Andiko hili limeandaliwa na wataalamu wa kitengo cha kilimo, mifugo na utunzaji wa mazingira wa Jeshi la Magereza linaeleza kuwa magereza yote 129 yanatarajia kunufaika," alisema.

Alieleza kuwa mradi huo kwa mchanganuo wa gesi vunde (vituo 50), gesi ya LPG (vituo 27), gesi asili (vituo 2) na mkaa mbadala unaotokana na makaa ya mawe yatatumika katika magereza yote na kambi zake.





# Viongozi ushirika watuhumiwa kuiba milioni 800/- za wakulima

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

BAADHI ya viongozi wa vyama vya ushirika vya wakulima wa kakao wilayani Kyela mkoani Mbeya, wanatuhumiwa kushirikiana na watunza maghala kuhujumu mfumo wa stahabadhi ghalani ambao unatumika kwenye ununuzi wa zao hilo kwa kutafuna zaidi ya Sh. milioni 800 za wakulima.

Viongozi hao wanadaiwa kuhujumu mfumo huo kwa kufanya mnada hewa wa zao hilo na kuchukua fedha za wanunuzi wanaoshinda kwenye mnada.

Juzi Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kuwakamata na kuwasweka ndani viongozi wa vyama vya ushirika na watunza maghala wa AMCOS zote ambazo zitabainika kushiriki kwenye uhuni huo.

Pia alitoa siku 14 kwa viongozi hao kuwalipa wakulima fedha zote wanazodai na kwamba wasiporejesha wataendelea kusota rumande na kuchukuliwa hatua kali zaidi za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani na endapo watarejesha wataachiwa huru.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kurejesha fedha hizo kwa awamu mbili ambazo awamu ya kwanza wanatakiwa kulipa Sh. milioni 400 ndani ya wiki ya kwanza na wiki ya pili wanatakiwa kumalizia Sh. milioni 400 zitakazobaki.

"Lakini kama wataamua kurejesha zote Sh.milioni 800 ndani ya wiki moja nitawaachia na naagiza Jeshi la Polisi anzeni nao sasa hivi, waliopo kamata nenda nao na wengine watafuata uchunguzi utakapokamilika," alisema Homera.

Aidha aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kufanya uchunguzi kwenye vyama vyote vya msingi katika wilaya hiyo ili kuwabaini wahusika wengine wanaohujumu mfumo huo ili waunganishwe na ambao wamekamatwa.

Vilevile aliagiza wawachunguze wanunuzi wa zao hilo kwa maelezo kuwa wapo baadhi yao pia wanashiriki kuhujumu mfumo kwa kununua kakao moja kwa moja kwa wakulima.

Kaimu Mkurugenzi wa mfumo wa stakabadhi gharani, Asangye Bangu, alisema walifanya uchunguzi wa hujuma hizo na kubaini kuwa viongozi hao baada ya kujipatia fedha hizo walikwenda kuponda raha katika maeneo mbalimbali ya starehe.

Alisema moja kati ya maeneo ambayo walikwenda kutumia fedha hizo ni katika fukwe za Ziwa Nyasa zilizoko katika wilaya hiyo ikiwamo Matema jambo ambalo linahatarisha ustawi wa mfumo huo wa stakabadhi ghalani.

Alisema baada ya kukamilisha uchunguzi walikabidhi taarifa TAKUKURU kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria na kwamba wanapendekeza wahusika wachukuliwe hatua kali za kisheria.

"Kilichofanyika ni makosa makubwa sana na waliokosewa ni Watanzania, hapa ni lazima tuchukuliane hatua kali, tusipofanya hivyo tutakuwa tunadidimiza uchumi wa wakulima wetu ambao wanatumia nguvu na rasilimali zao kwenye uzalishaji," alisema Bangu.

Alisema moja ya madhara ya hujuma hiyo ni viongozi wachache kujilimbikizia mali wakati wakulima wanaotumia rasilimali zao wanaendelea kuwa masikini.

Alisema kwenye uchunguzi wao walibaini pia baadhi ya wafanyabiashara kushirikiana na viongozi wa AMCOS na watunza maghala kuhujumu mfumo huo.

Baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika wilayani humo waliwalalamikia wasimamizi wa maghala kuharibu utaratibu kwa kutotoa risiti kwa wateja wakisingizia kukatika kwa umeme katika maeneo yao jambo ambalo linahatarisha upotevu wa mali.

Wilaya ya Kyela ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa kakao nchini na ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya mapato ya Halmashauri ya Kyela ambapo kwa sasa kilo moja ya zao hilo inauzwa kati ya Sh. 5,000 na 8,000.



Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (wa pili kushoto), akikagua na kuonja vyakula vilivyoandaliwa na baadhi ya mamantilie wa Wilaya ya Rungwe juzi, wakati wa uzinduzi wa Tamasha la Mama Ntilie lililoanzishwa kwa lengo la kuwawezesha mitaji na mafunzo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Naibu Waziri aagiza ujenzi shule mpya ufanyike usiku, mchana

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratias Ndejembi, ameagiza ujenzi wa shule mpya ya sekondari inayojengwa katika Kijiji cha Mbugani Kata ya Kitandililo Halmashauri ya Mji Makambako mkoani Njombe yenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 500 kufanyika usiku na mchana ili ukamilike haraka.

Ndejembi alilitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea ujenzi huo ambao unatekelezwa kupitia mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari nchini (SEQUIP) na kubaini kuwa unasuasua na kuagiza muda wa kufanya kazi uongezeke ili majengo hayo yakamilike kwa muda unaotakiwa.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), Dk. Charles Msonde, aliahidi kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa shule hizo mpya nchi nzima ili kuhakikisha Oktoba 31 mwaka huu, shule zote za SEQUIP ziwe zimekwisha.

Awali Mbunge wa Makambako ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Njombe, Deo Sanga pamoja na Diwani wa Kata ya Kitandililo, Iman Fute walikiri mapungufu na walimwomba Naibu Waziri kuwaongezea muda.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kitandililo, Albert Kahonga, alisema serikali imetoa zaidi ya Sh.milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ili kuwaondolea wanafunzi changamoto ya kutembea umbali mrefu.

**Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), Dk. Charles Msonde, aliahidi kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa shule hizo mpya nchi nzima ili kuhakikisha Oktoba 31 mwaka huu, shule zote za SEQUIP ziwe zimekwisha.**

# Wanawake 700 mkoani Mbeya kupewa majiko ya gesi

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ameahidi kugawa majiko ya gesi kwa wanawake zaidi ya 700 mkoani Mbeya ili kuwasaidia kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Aliyasema hayo wilayani Rungwe alipokuwa anazindua tamasha la mama ntilie ambalo linalenga kuwashindanisha mama ntilie kwenye mapishi ya vyakula vya aina mbalimbali pamoja na kuwawezesha mitaji kwa ajili ya shughuli zao.

Alisema mbali na kuwasaidia wanawake kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa, pia analenga kuwasaidia kwenye utunzaji wa mazingira kwa maelezo kuwa nishati ya gesi haichafui mazingira na wala haichochei ukataji wa miti.

Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, alisema mitungi hiyo atagawa kwa wanawake wa halmashauri zote saba za mkoa huo ambazo kila halmashauri watanufaika wanawake 100.

Aliwaomba wabunge wa majimbo mengine ya mkoa huo kumuunga mkono kwenye utoaji wa zawadi hizo ili wanawake wengi zaidi waongezewe mitaji.

Aidha, aliwashukuru wadau mbalimbali ambao wamemuunga mkono kwenye tamasha hilo zikiwamo kampuni za uzalishaji na usambazaji wa gesi ya kupikia.

Mwakilishi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Mkoa wa Mbeya, Rajab Ghuliku, alisema washindi wa kwanza katika kila halmashauri watapatiwa mafunzo maalumu na chuo hicho ili wabobee kwenye mapishi.

Alisema washindi hao pia watafundishwa namna bora ya kuandaa chakula katika hatua zote ili waongeze thamani ya biashara yao ikiwamo maarifa ya usafi wa chakula.

"Tutawafundisha kwa muda wa miezi mitatu na lengo kuu ni kuhakikisha wanakuwa na maarifa ya kuandaa chakula chenye ubora na usafi wa hali ya juu," alisema Ghuliku.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Mbeya, Edna Mwaigomole, alimshukuru Naibu Waziri huyo kwa kulisaidia kundi hilo akidai kuwa ndilo limekuwa likiathirika zaidi na matumizi ya nishati chafu.

Alisema ugawaji wa mitungi ya gesi ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo inasisitiza matumizi ya nishati safi ambayo inachochea utunzaji wa mazingira.





# Sheria ya Uvuvi kufumuliwa iendane na kasi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu imesema ipo katika mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Uvuvi ili iweze kwenda na kasi ya uchumi wa buluu na kulinda rasilimali za baharini pamoja na kupambana na uvuvi haramu na mazalia ya samaki.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, wakati akizungumza na wavuvi wa maeneo ya ghuba ya Chwaka kuhusu hatua za serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Uvuvi Namba 7 ya Mwaka 2010 ili kwenda na wakati kukabiliana na uvuvi haramu ambao ni tishio.

Alisema Zanzibar inatekeleza sera ya uchumi wa buluu ambayo sehemu ya malengo yake makubwa ni kulinda rasilimali za baharini ikiwamo matumbawe pamoja na samaki.

Alisema bado uvuvi haramu unaendelea katika mwambao wa Unguja na Pemba kwa kutumia mitego hatari pamoja na mishale (bunduki) ambayo uharibu matumbawe.

Aidha, aliitaja baadhi ya aina ya uvuvi haramu unaotumika ni pamoja na nyavu zenye macho madogo ambazo hunasa samaki wa aina zote ambao hawafai kwa matumizi ya kula.

"Wizara yetu inatekeleza sera ya uchumi wa buluu ambayo ni kulinda rasilimali za baharini ikiwamo matumbawe na samaki kwa hivyo tupo katika mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Uvuvi itakayokwenda na wakati wa dunia uliopo sasa," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi, Dk. Salum Soud Mohamed, alisema wamebaini kuwa baadhi ya wavuvi wanavua samaki wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula kwa kutumia mitego yenye macho madogo.

Alisema Sheria ya Uvuvi ya sasa inapiga marufuku uvuvi wa aina hiyo ambayo inataka kutaifishwa nyavu za aina hiyo.

Mkuu wa Hifadhi ya Ghuba ya Chwaka, Ali Haji Simai, alisema wameanza kutumia sheria ndogo kwa wavuvi wote ikiwamo kufungia kwa muda baadhi ya aina ya uvuvi ikiwemo pweza pamoja na ngisi.

Alisema tayari makubaliano yamefikiwa kwa wavuvi kutoka Michamvi na wenzao wa Uroa kuacha kulitumia eneo la ufukwe wa Michamvi kwa muda wa miezi minne ili kutoa nafasi ya kuzaliwa kwa samaki aina ya ngisi na pweza.

# Zanzibar yaanza kufanya utafiti wa madini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar kwa kushirikiana na Kampuni ya Aseel Oilfield wanatarajia kufanya utafiti wa awali wa madini visiwani hapa.

Akizungumza visiwani Zanzibar, katika hafla ya uzinduzi wa utafiti huo ambao unatarajiwa kuanza kesho, Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaaban Ali Othman, aliitaka kampuni inayofanya utafiti huo kuhakikisha matokeo 'data' na taarifa zote zitakazopatikana katika utafiti zinakuwa siri na zinapelekwa serikalini.

Alisema taarifa za utafiti huo hazipaswi kutolewa nje ya serikali na ni kosa kwa mujibu wa makubaliano yao kwa kampuni hiyo.

"Kampuni hii imejiaminisha kufanya utafiti lakini haimaanishi taarifa zinazopatikana ni mali yao bali ni mali ya serikali," alisema.

Aidha, alisema lengo la serikali kuingia makubaliano na kampuni hiyo ni kutafuta vyanzo vingine ambavyo vitaongeza uchumi wa nchi.

"Zanzibar kwa kipindi kirefu tulikuwa tunategemea karafuu lakini kila sehemu zinalimwa. Hata katika soko la dunia, Zanzibar hatupo peke yetu, utalii nao kila nchi inautaka hivyo ni lazima kuingia katika sekta ya madini na tusibaki kwenye mchanga, kokoto na kifusi pekee ili kuangalia ardhi yetu ina kitu gani," alisema.

Naibu waziri huyo alisema kuwa wizara yake itahakikisha inatoa kila aina ya ushirikiano ili kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa na kuahidi kufanya mikutano na viongozi wa mikoa, wilaya, shehia na wananchi katika maeneo yote ya Unguja na Pemba ili kutoa ushirikiano wakati kampuni hiyo inapofanya utafiti.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Kilangi, alisema lengo la serikali ni kuja na kitu kipya ili kiweze kusaidia katika kuendelea kukuza maendeleo ya nchi.

Alisema serikali imeweka mazingira rafiki kwa wawekezaji kuwekeza Zanzibar katika sekta mbalimbali, ambapo wizara yao imeanza kupokea wawekezaji kupitia sekta ya madini na nishati.

Aidha, alisema ujio wa ushirikiano huo ni mafanikio makubwa ambayo yatawawezesha kufanya utafiti Unguja na Pemba ili kubaini Zanzibar ina madini ya aina gani, wingi wake, thamani na yatafanyiwa kazi gani.

Kilangi alisema Zanzibar imekuwa ikifanya utafiti mbalimbali ikiwamo za gesi, mafuta miamba na tafiti nyingine, hivyo kampuni hiyo itasaidia kurahisisha zoezi la kuchambua miamba iliyokuwapo Unguja na Pemba.

Hivyo, aliwahakikishia wananchi kwamba utafiti huo hauna uhusiano na ardhi ya mtu bali serikali inataka kutambua kilichokuwapo chini ya ardhi na sio jambo lingine.

Mwenyekiti wa kampuni hiyo, Iman Al -Jabry, alisema kampuni yake ipo tayari kwa kufanya utafiti huo na wataifanya kazi hiyo kwa muda wa miezi minne na wataifanya kwa ufanisi na weledi.

Alisema utafiti huo utakapofanikiwa utabadilisha maisha ya wananchi na kukifungua kiuchumi kisiwa cha Zanzibar na kupata maendeleo endelevu.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (wa pili kushoto), akizungumza na Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Hassan Ali Hassan, alipofanya ziara katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume jana, kuangalia utendaji wa idara hiyo, katika kuwahudumia wageni wanaofika nchini. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jeshi la Uhamiaji laagizwa kufanya kazi kwa ufanisi, weledi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, amesema viwanja vya ndege ndiyo milango mikuu ya uchumi wa nchi kutokana na wageni na watalii wengi kutumia viwanja hivyo.

Hivyo aliliitaka Jeshi la Uhamiaji kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa ufanisi, weledi na uwadilifu katika viwanja hivyo kwa sababu serikali inachukua hatua za kutengeneza fursa nyingi kwa utalii, uwekezaji na kuimarisha biashara.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar baada ya kufanya ziara katika viwanja vya ndege vya Abeid Amani Karume Zanzibar na kuzungumza na watendaji wa Jeshi la Uhamiaji Zanzibar.

Masauni alisema watalii na wawekezaji wanaofika nchini kwa shughuli za kiuchumi, wanategemea kupita katika maeneo hayo ya viwanja vya ndege, hivyo Jeshi la Uhamiaji wanapaswa kutoa huduma nzuri.

Alisema anafahamu uwepo wa changamoto mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao na ndio maana ameamua kufanya ziara hiyo ili kujiridhisha na kupokea taarifa ili kuimarisha ufanisi katika maeneo hayo katika kutoa huduma bora.

"Nimekuja hapa zipo changamoto ambazo ni za kimifumo na tunazichukua na kuzifanyia kazi, pia zipo changamoto za kiutawala ambazo tushazitolea maelekezo lengo kuhakikisha askari yoyote wa uhamiaji kutekeleza kazi zake kwa weledi na uwadilifu," alisema. Aidha, alisema lazima Jeshi la Uhamiaji kuhakikisha mapato ya serikali yanayotegemewa kupitia viwanja vya ndege yanaendelea kudhibitiwa.

"Tunaposhughulika na vyombo vya usalama tusitegemee kuwa mambo yote tutayasema hadharani itoshe kueleza hayo niliyoyaeleza na serikali ipo makini sana katika kusimamia rasilimali zake fedha iwe kuna changamoto ya kimifumo au kiuwadilifu tunakwenda kudhibiti na kupambana nayo," alisema.

Naye Kamishna wa Jeshi la Uhamiaji Zanzibar, Hassan Ali Hassan, alisema licha ya kujitahidi kufanyakazi ya kuwahudumia wageni lakini wanakabiliwa na changamoto za kimifumo katika kuwahudumia watalii na wageni katika uwanja huo wa ndege.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**MHINDI NESI NGUSA** anatangaza kupotea kwa **RESULT SLIP** yenye index namba **P2336-0064** iliyotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BRITISH SCHOOL** mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/19052/2023**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**AMINA MOHAMED** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3678-0005** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MIKANJUNI SEKONDARI** mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **BUG/W/A.16/14/VOL.XX1**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo KISARAWE**

**Kituo cha KISARAWE Mkoa wa PWANI**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 22/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HILLARY MOHAMED SULEMAN WA MAKURUNGE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HERMAN JOSEPH MGOMBERE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 mwezi 10 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
**Imetokewa leo tarehe 09 mwezi 10 mwaka 2023.**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO
KISARAWE

## KUPOTELEWA NA CHETI



**BRIAN DAMIAN KAIJANANTE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2732/0112** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MNADANI SEKONDARI** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/177670/2023.**

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**YAH: KIWANJA NA.3 KITALU '222' NGAMIANI JIJINI TANGA**

**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB NA. S.47694**

**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA ALLY ABDALLAH,**
**S.L.P 178,**
**TANGA**

**MUOMBAJI: JUMBE ALLY ABDALLAH (msimamizi wa Mirathi ya ALLY ABDALLAH)**
**S.L.P 178,**
**TANGA**

Taarifa inatolewa kwamba: Barua ya toleo ya kumiliki kiwanja kilichotajwa hapo juu imepotea. Hivyo basi ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja tangu tarehe ya taarifa hii kutangazwa katika gazeti.
Barua halisi ys toleo ikipatikana irudishwe kwa **MKURUGENZI WA JIJI wa S.L.P 178 TANGA**

Wendeline Izina
Kny: MKURUGENZI WA JIJI

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DAUDI MBOTA SABAI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 349 BQU.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/TAN/MUH/1591/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISRAEL MATHAYO SHALAMANZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 264 DUM** aina ya **Toyota IST**. Chassis No. **NCP600219350,** Engine No. **2NZ3657221.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi namba
**DOD/DOD/RB/106794/2023**

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**MODESTUS MARTIN LUMATO** anatangaza kupotea kwa ofa ya umiliki wa kiwanja **Plot 93 block H Itega – Dodoma.** yeyote atakayeiyona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/DOD/DOD/5101/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARY IMINZA INZOFU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 886 BNW,** CHASSIS NAMBA: **AZR600003139** na ENGINE NAMBA: **1AZ4089215.** Kwa yeyote atakakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI
**TAARIFA:ARU/ARU/RB/272241/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 130/ 2023**

**In the matter of the Estate of the late TEONILA ALPHONCE MGULUNDE of NJEDENGWA EAST within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SAMUEL NIKWANDUKA MTAWA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 31 Day of 10,2023

Date at Dodoma this 29th Day of SEPTEMBER, 2023

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT
RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA TRAILLER

**TEMBA FILLING STATION TOURS AND TRANSPORT CO. LTD** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 412 DCS** aina ya SCANIA yenye Chassis No. **5181470.** Kadi ya Trailler yenye namba za usajili **T 414 DCS** yenye chassis No. **NP9BT22WAE3025039.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DAR/KIN/23810/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya MUFINDI**

**Kituo cha MAFINGA Mkoa IRINGA**

**Shauri la Madai Na 28/2023**

**Jina la mdai MUCOBA BANK PLC (EMANUEL CHENGULA)**

**Jina la mdaiwa BONIFACE CHUMO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa BONIFACE CHUMO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa za madai)
MADAI YA Tsh. 8,900,406.91/= YATOKANAYO NA MKOPO
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii
Tarehe 13 mwezi 10 mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelzo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 3 mwezi 10 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MAFINGA
WILAYA YA MUFINDI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA MADAI RUFAA NA 3 YA 2023**
**SHAMBO SHIRIKISHO.......... MRUFANI**
**DHIDI YA**
**NGASSA LUHENDE GODI.........MRUFANIWA**
**KWA: NGASSA LUHENDE GODI; -**

**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**
Unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 27/10/2023 siku ya IJUMAA saa 3:00 asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA ukikosa siku hiyo, Hukumu itatolewa upande mmoja bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 4/10/2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

## KUPOTEA KWA LESENI YA UCHIMBAJI MADINI

**SWEDI FARAJI MSANGI ANATANGAZA KUPOTEA KWA LESINI YA UCHIMBAJI MADINI YENYE NAMBA YA USAJILI PML00334SMN KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA PHQ/ARU/ARU/1676/2023**

*OFISI ZA MATANGAZO*
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Balozi Kallua: Watanzania wako salama

**TEL AVIV,** Israel

BALOZI wa Tanzania nchini Israel, Alex Kallua, amesema taifa hilo limewahakikishia kwamba litaendelea kulinda usalama wa raia pamoja na wananchi wote wanaoishi katika taifa hilo la Israel.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari, Balozi Kallua, alisema kuwa jana walilala salama bila kusikia tukio lolote wala milipuko, akieleza kuwa kama kulikuwa na mashambulizi basi yatakuwa yamekingwa kutokana na mfumo wa ulinzi uliopo.

"Naomba niwatoe hofu wazazi na Watanzania wenzangu, mbali na Watanzania wenzetu wawili ambao hatuna taarifa nao na hatudhani kwamba kuna mabaya kabisa yamewatokea tunahisi kwamba sababu ya mtafaruku na hali ilivyokuwa katika maeneo ya Israel wanayoyakomboa pengine walijificha kwenye maeneo hayo," alisema na kuongeza:

"Lakini Watanzania wengine wote wako salama na tumeambiwa tuendelee kukaa kwa utulivu wakati serikali ikichukua hatua stahiki kuhakikisha usalama unarejea kikamilifu katika taifa hili," alisema Balozi Kallua.

**KINACHOENDELEA**

Siku nne baada ya Hamas wa Palestina kuishambulia Israel, Jeshi la Israel, (IDF) lilisema limechukua tena udhibiti wa uzio wa mpaka wa Gaza.

Kwa mujibu wa maoni yaliyorushwa na kituo cha Radio ya Jeshi la Israel na kunukuliwa na Shirika la habari la Reuters, Msemaji Mkuu wa Jeshi la Israel Daniel Hagari, alisema vikosi vya taifa hilo vinategea mabomu ya ardhini katika maeneo ambako uzio ulivunjwa.

Aliongeza kuwa tangu juzi hakukuwa na uvamizi mpya kutoka Gaza kunakotawaliwa na Hamas na kwamba IDF linazidi kujiimarisha kwenye eneo hilo dhidi ya uvamizi wa aina yoyote.

"IDF imedhibiti kikamilifu eneo linalozunguka Ukanda wa Gaza. Hakukuwa na uvamizi wowote wa magaidi usiku wa kuamkia leo, 'jana' kulingana na kile tunachokijua. Sera yetu ya kufyatua risasi kuelekea kwenye uzio inamaanisha kwamba mtu yeyote anayekaribia uzio huo atauawa," alisema.

Aidha, Israel ilieleza kuwa imepeleka vifaru kwenye mipaka na Lebanon katikati ya wasiwasi wa kuongezeka kwa mzozo baada ya kuishambulia Lebanon na kuwaua karibu wanamgambo watatu wa Hezbollah.

**UN**

Naye Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, alisema wananchi wanaoishi Ukanda wa Gaza wanakabiliwa na hali mbaya, huku akitoa wito kwa Israel kuheshimu sheria za kimataifa, wakati ikifanya operesheni zake za kijeshi katika ukanda huo.

Guterres alieleza kufadhaishwa na tangazo la Israel kuwa ingeweka mzingiro kamili dhidi ya ukanda huo, ikizuia kikamilifu kuingizwa kwa chakula, maji na nishati ya umeme.

"Natambua uhalali wa wasiwasi wa Israel kuhusu usalama wake," alisema.

Wakati huo huo Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, alisema vita baina ya Israel na Hamas havipaswi kuchochea zaidi moto wa uhasama, akieleza kuwa ugaidi hautashinda.

Akiwa pamoja na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, mjini Hamburg, viongozi hao wawili walisema wanasimama pamoja na Israel. Aidha, wakati hayo yakijiri Umoja wa Ulaya (EU) umefuta kauli yake ya awali kuwa unasitisha msaada wa kibinadamu kwa Wapalestina.

Naye Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, aliutaka upinzani nchini mwake kuridhia kuundwa kwa serikali ya umoja wa kitaifa bila masharti yoyote, wakati nchi hiyo ikiendelea na operesheni za kulipa kisasi dhidi ya Hamas.

Ilibainishwa kuwa zaidi ya siku mbili baada ya Hamas kuanzisha mashambulizi ya kushtukiza kutokea Ukanda wa Gaza, jeshi la Israel limesema kwa kiasi kikubwa limerudisha udhibiti katika miji ya kusini ambako limekuwa likipambana na Hamas. **DW**

## Operesheni kurekebisha maumbile yaja

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili Tawi la Mloganzila, inatarajia kuanzisha huduma ya kurekebisha maumbile na mwonekano wa mwili yakiwamo matiti.

Mkuu wa Idara ya Upasuaji MNH - Mloganzila, Dk. Eric Muhumba, alisema jana kuwa huduma hiyo itaanza kutolewa kuanzia Oktoba 27, mwaka huu.

"Ninaomba kuuarifu umma wa Watanzania kuanzia tarehe 27, mwezi huu, kutakuwa na upasuaji wa kibingwa wa kupunguza uzito na kufanya upasuaji rekebishi. Huu utakuwa upasuaji wa kwanza kufanyika Tanzania,"alisema.

Dk. Muhumba alisema wanaposema upasuaji wa kupunguza uzito wanamaanisha kwamba ni upasuaji unaofanyika kwenye tumbo kwa kupunguza nafasi ya kuhifadhi chakula. Alisema katika operesheni hizo ziko za aina tatu ambazo ni kupunguza tumbo lenyewe kwa kukata sehemu ya tumbo au kuvuka sehemu ya kuhifadhia chakula na kukifanya kikitoka kwenye koo kwenda moja kwa moja katika utumbo mdogo.

Alitaja aina nyingine kuwa ni kwa kulishona tumbo na kubaki nafasi kidogo.

"Operesheni zote hizi zitafanyika. Kuhusu upasuaji rekebishi ni kupunguza mafuta katika tumbo au mama anataka kurekebisha matiti yake madogo au makubwa vyote vitafanyika au mkono umejaa nyama utarekebishwa.

"Huduma hii ya upasuaji rekebishi au kupunguza uzito hospitali hapa gharama zake itakuwa nafuu kwa kulinganisha na zile za nje ya nchi," alisema.

Dk. Muhumba alisema huduma inayofanyika nje ni hapa, matokeo yake ni sawasawa kinachotofautiana ni gharama.



Mwanajeshi wa Israel akiendesha kifaru katika eneo la mpaka wa Gaza kusini mwa Israel, ikiwa ni juhudi za kuimarisha ulinzi katika eneo hilo, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Kifo cha DMO 'gesti' chazua utata

**Na Mwandishi Wetu**

MGANGA Mkuu wa wilaya ya Moshi (DMO) mkoani Kilimanjaro, Dk. Alex Kazula, amefariki dunia akiwa katika nyumba ya kulala wageni huku kifo chake kikigubikwa na utata.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 9, katika moja ya nyumba za wageni (jina halijatajwa).

"Tulipokea taarifa za kifo cha mtumishi huyu wa Moshi Vijijini, tunaendelea na uchunguzi kujua chanzo cha kifo hicho," alisema Kamanda Maigwa.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makore, alisema Dk. Alex alifariki usiku wa kuamkia Jumatatu (Oktoba 9), na kuongeza kuwa uchunguzi wa tukio hilo unaendelea.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Shedrack Mhagama, alithibitisha taarifa hizo na mtumishi huo ataagwa leo nyumbani kwake ambako ni nje ya ofisi ya halmashauri.

Alisema baada ya kuaga mwili huo utasafirishwa kwenda nyumbani kwao mkoani Iringa.

"Kwenye siku za mwisho wa wiki alikuwa na watu wanne ambao walimpeleka eneo fulani na mmoja akachukua simu yake na baadaye walipewa taarifa za msiba, hatutaki kusema sana hilo eneo kwa sababu suala hili liko kwenye vyombo vya uchunguzi na taarifa na wangapi waliokuwa naye wamekamatwa polisi ndio watasema, ila tunajua wameshikiliwa," alisema.

Baadhi ya mashuhuda ambao hawakutaka kutajwa majina yao walisema ndani ya chumba hicho waliona kinyesi na damu hali inayoashiria huenda alinyongwa.

Nipashe ilifika nyumbani na kuzungumza na baadhi ya majirani ambao walikataa kutajwa majina yao na kusema kuwa bado tukio hilo lina utata mkubwa.

"Sawa inaweza kuwa mapenzi ya Mungu, lakini hiki kifo kina utata sana. Tunasikia huyu kaka amekuwa na watu wanao husika kwenye ofisi yake. Wiki iliyopita wapo watu ambao hatujui wametoka taasisi gani walileta vitenganishi na vifaa tiba alivikataa kutokana na kukosa ubora, sasa upo uwezekano wamemuua," alidai.

Hata hivyo, familia yake haikuwa tayari kuzungumza kifo hicho.

Katika ubao wa matangazo wa Halmashauri ya Moshi lilionekana tangazo la kifo cha mtumishi huyo.

Jirani yake ambaye ni mtumishi mwenzake alisema kuna utata kwenye tukio hilo kwa kuwa wiki chache zilizopita kuna vifaa tiba na vitenganishi vililetwa akavikataa kwasababu havikukidhi viwango.

"Tunapata shaka sana na hili tukio kwa kuwa hivi vifaa vilikuja na huyu alivikataa," alisema jirani huyo ambaye jina lake limehifadhiwa.

Mwandishi alimtafuta mwanafamilia aliyekutwa nyumbani kwa marehemu na alimjibu kuwa hawezi kusema lolote kwa sasa.

DMO huyo ambaye mkewe alishafariki, alikuwa anaishi na dada yake, mjomba wake, watoto wake na msichana wa kazi ambao hakuna aliyekubali kuzungumza lolote kuhusu kifo hicho.

# JKT QUEENS YAJIPA NAFASI KUNDI A LIGI YA MABINGWA

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya JKT Queens umesema lengo lao ni kutinga hatua ya fainali kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake iyotarajiwa kuanza kutimua vumbi Novemba 5-19, mwaka huu nchini Ivory Coast.

Katika michuano hiyo, JKT Queens imepangwa Kundi A pamoja na wenyeji wa michuano hiyo, Athletico FC, Sporting Casablanca (Morocco) na mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Msemaji wa timu hiyo, Masau Bwire, alisema hawazihofii timu walizopangwa nazo katika kundi hilo kutokana na ubora wa kikosi chao kwa sasa.**

"Hatuna hofu na kundi tulilopangwa kwani tunaimani na kikosi chetu pamoja na benchi la ufundi lililopo kwa sasa," alisema Masau Bwire.

Aliongeza kuwa kila mchezaji ana morali ya kwenda kuipigania timu na kuiwezesha kusonga mbele katika mashindano hayo ambayo alikiri kuwa yatakuwa na ushindani mkubwa.

Aidha, aliwaomba Watanzania wawaunge mkono ili waweze kwenda kutimiza malengo yao hayo huku akiwataka waondoe shaka kuhusu timu walizopangwa nazo katika kundi lao.

Alisema kwa sasa timu yao ipo kambini na tayari wamecheza michezo mbalimbali ya kirafiki ili kuimarisha uwezo wa kila mchezaji.

"Asilimia 75 ya wachezaji wetu wapo kwenye kambi ya timu ya taifa ambayo inajiandaa na mchezo dhidi ya Botswana utakaochezwa Oktoba 26, mwaka huu, hapa Dar es Salaam, baada ya kumaliza mchezo huo wa marudiano Botswana, ifikapo Oktoba 30, wataondokea huko huko kuelekea nchini Ivory Coast," alisema Bwire.

**KIKAPU...**



Timu ya Wafanyakazi wa Mohamed Enterprises ya Mpira wa Kikapu, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Minziro awafungia kazi mabeki*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Prisons, Fred Felix Minziro, amesema kipindi hiki cha mapumziko atakuwa na kazi moja tu ya kurekebisha makosa ambayo mabeki wake wanayafanya kiasi cha kuruhusu mabao karibuni kila mechi.

Minziro amekiri kuwa idara yake ya ulinzi inahitaji marekebisho ya hali ya juu na yeye kama kocha ana jukumu la kuwaelekeza nini cha kufanya ili kutorudia tena pale watakapoivaa JKT Tanzania, Oktoba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Prisons ndiyo timu inayoongoza kuruhusu mabao mengi kwenye Ligi Kuu mpaka kufikia raundi ya 15, ikiwa imeshapachikwa mabao 11, ikifuatiwa na Mtibwa Sugar iliyoruhusu mabao 10.

"Tumeanza vibaya ligi kwa sababu tulikuwa na maingizo mengi ya wachezaji wapya, tuliingiza damu changa na mechi za kwanza ilikuwa kwa ajili ya kuwapa uzoefu, tulikuwa na matatizo kwenye ufungaji na uzuiaji, lakini baadaye kila mechi ambayo tulikuwa tukipoteza tunapata bao, hapo nikaona kuna mwanga.

"Lakini bado napambana sana kwenye idara ya ulinzi, nataka wasiwe wanaruhusu mabao kwani hata mechi ya mwisho tuliyoshinda bado tuliruhusu mabao mawili, ila kwa kipindi hiki cha mapumziko nitafanya kazi kubwa ya kupambana nalo, nadhani tunavyozidi kwenda mbele makosa haya yatapungua na baadaye yataisha kabisa," alisema Minziro.

Jumapili iliyopita, Prisons ilipata ushindi wake wa kwanza ikiifunga Mtibwa Sugar mabao 3-2, lakini kabla ya hapo ilipitia vipigo, cha mabao 3-1 dhidi ya Azam FC, Tabora United na Simba, huku ikitoka suluhu moja dhidi ya Singida Fountain Gate.

Akizungumzia tathmini ya Ligi Kuu mpaka kufikia raundi ya tano alisema ni ligi yenye mvuto, ngumu na nzuri kutokana na upinzani unaoonyeshwa na timu mbalimbali ambazo zimejitahidi kufanya usajili mkubwa wenye wachezaji bora.

"Ligi ya mwaka huu ni nzuri na ngumu, unaona hata baadhi ya matokeo kwa baadhi ya timu zile tulizozizoea kushinda siyo mazuri sana, na hii ni mwanzo tu, huko tunakokwenda tutarajie matokeo mengine ambayo hayatarajiwi," alisema beki huyo wa pembeni wa zamani wa Yanga miaka ya 1980.



# Singida FG kuamua Gomes au Pablo

**Na Saada Akida**

KLABU ya Singida Fountain Gate FC, inatarajia kumtangaza kocha wake mkuu Jumamosi wiki hii, huku majina ya makocha wa zamani wa Simba, Pablo Franco Martin na Didier Gomes da Rosa (pichani), yakitajwa ni miongoni mwa makocha waliotuma wasifu wao kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Mjerumani Ernst Middendorp.

Awali, uongozi wa Singida Fountain Gate FC kupitia kwa rais wa klabu hiyo, Japhet Makau, alitangaza kabla ya kukutana na Simba wangemtangaza kocha huyo anayekuja kukinoa kikosi cha timu hiyo, lakini ratiba imebadilika kutokana na taratibu za kiutawala.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa timu hiyo, Hussein Masanza, alikiri kuwa walikuwa na mpango wa kumtambulisha kocha mapema kabla ya kucheza na Simba, lakini mazungumzo bado hayajakamilika na wanaendelea kupitia CV (wasifu) za makocha wengi.

Alisema Gomes na Pablo ni miongoni mwa makocha zaidi ya 100 walituma CV zao na wako katika mazungumzo kuangalia ni kocha yupi anaweza kuwafikisha katika malengo.

"Tumekuwa na majadiliano na makocha mbalimbali, tunahitaji kupata kocha ambaye atakuwa juu na si timu kuwa juu yake, tunatarajia hadi wiki hii tutamtangaza kocha wetu awe Gomes au Pablo hilo litajulikana siku hiyo.



"Tunahitaji hadi tunapokwenda Ruangwa, Lindi kucheza dhidi ya Namungo FC, Kocha Mkuu ameshapatikana na tumemtangaza rasmi kuwa sehemu ya benchi la ufundi," alisema Massanza.

Kuhusu kikosi, alisema wachezaji wamepewa mapumziko ya siku tatu, na kesho wataingia kambini kujiandaa na mechi yao ijayo dhidi ya Namungo FC.

"Ninaimani baada ya kurejea wachezaji ambao hawako kwenye majukumu ya timu ya taifa, wataingia kambini na tunatarajia kutafuta timu ya kucheza mechi moja ya kirafiki kwa kipindi cha siku 10 timu inapokuwa kambini," alisema Massanza.

Singida Fountain Gate FC wanatarajia kusafiriki kwenda Ruangwa, Lindi kukabiliana na wenyeji wao, Namungo FC Oktoba 22, mwaka huu, kwenye dimba la Majaliwa, mkoani humo.

## ZISIKUPITE

### ROONEY KUINOA BIRMIGHAM

MSHAMBULIAJI wa zamani wa England, Wayne Rooney, amekubali dili la kuinoa Birmingham City kwa mshahara ambao ni mara tatu zaidi ya John Eustace aliokuwa nao kabla ya kutimuliwa na timu hiyo ya Championship. ***(Times)***

### VINICIUS MKATABA MPYA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Vinicius Jr, bado hajasaini mkataba mpya na Real Madrid, huku mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ukikamilika msimu ujao wa majira ya joto. ***(Sport)***

### GATTI KUONGEZA MKATABA

BEKI wa Juventus, Federico Gatti mwenye umri wa miaka 25, ataongeza mkataba wake na klabu hiyo hadi mwaka 2028 baada ya kurejea kutoka katika majukumu ya kimataifa na Italia. ***(Tuttosport, via Tuttomercatoweb)***

### SIMEONE AIKUBALIA ATLETICO

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone mwenye umri wa miaka 53, amekubali kwa mdomo kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Hispania. ***(Fabrizio Romano)***

### BECKHAM KUPEWA UBALOZI

KIUNGO wa kati wa zamani wa Manchester United na England, David Beckham mwenye umri wa miaka 48, atapewa wadhifa wa ubalozi katika klabu hiyo ya Old Trafford iwapo itachukuliwa na Sheikh Jassim bin Hamad Al Thani. ***(talkSPORT)***.

### KURUHUSIWA KUONDOKA

CHELSEA itamruhusu mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo AS Roma kuondoka kwa takriban pauni milioni 37 msimu ujao. ***(Fabrizio Romano)***

### DIER KUREJESHWA LISBON

KLABU ya Sporting Lisbon inaweza kuchukua hatua ya kumrejesha beki wa England, Eric Dier mwenye umri wa miaka 29, katika klabu hiyo Januari au mkataba wake utakapokamilika msimu ujao wa majira ya joto. ***(Times)***

### KANE NA BAYERN MUNICH

RAIS wa Heshima wa Bayern Munich, Uli Hoeness, amesema klabu hiyo ya Ujerumani ililipa pauni milioni 82 kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 30, kutoka Tottenham Hotspur msimu wa majira ya joto badala ya pauni milioni 85 pamoja na nyongeza. ***(BR24)***

### GARCIA KUBAKI NAPOLI

RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis, yuko tayari kuendelea na Kocha Mfaransa Rudi Garcia, ambaye yupo kwenye presha kubwa baada ya klabu hiyo kuanza vibaya msimu huu. ***(Soccer Italia)***

### WAKUMRITHI GARCIA

KOCHA wa zamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter, ni mmoja kati ya majina matatu, pamoja na Mcroatia Igor Tudor na Muargentina Marcelo Gallardo, ambao Napoli inaweza kuwateua iwapo watamtimua Rudi Garcia. ***(Foot Mercato)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SANCHO SASA KUONDOKA RASMI MANCHESTER UNITED

**MANCHESTER,** England

**Ten Hag alimtaka kuomba msamaha, lakini hadi sasa amegoma hivyo...**

MUDA wa Jadon Sancho kuomba msamaha kwa kocha Erik ten Hag unaelekea kumalizika pale Manchester United na kwamba sasa ni wazi kuwa anaelekea mwisho pale Old Trafford, kwa mujibu wa ESPN.

**Sancho bado hajaomba msamaha baada ya kudai kuwa Ten Hag alidanganya hadharani kuhusu sababu za yeye kuachwa kabla ya kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Arsenal Septemba 3, mwaka huu.**

Ten Hag alimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kuomba msamaha, lakini hadi sasa amekataa kufanya hivyo.

Ten Hag hajafunga kabisa mlango juu ya uwezekano wa Sancho kujumuishwa kwenye kikosi, lakini anatakiwa kwanza kuomba msamaha baada ya chapisho lake kwenye mtandao wa kijamii.

Sancho amebakia kwenye programu ya mazoezi ya mtu binafsi katika kambi ya mazoezi ya United kule Carrington na ana mwingiliano mdogo na wachezaji wenzake wa kikosi cha kwanza.

Jumamosi, alitazama timu ya vijana chini ya umri wa miaka 18 pale Carrington wakati timu ya kwanza iliwasili Old Trafford kabla ya ushindi wao wa mabao 2-1 dhidi ya Brentford.

Sancho, ambaye alisajiliwa kwa pauni milioni 73 kutoka Borussia Dortmund mwaka 2021, yuko chini ya mkataba hadi mwaka 2026 na kuna wasiwasi katika klabu kuhusu hali ya kifedha ambayo inaweza kuwa muhimu ili kuwezesha kuondoka kwake.

Thamani yake sokoni imeshuka kwa kiasi kikubwa baada ya misimu miwili iliyokatisha tamaa pale United na klabu chache sana duniani zinaweza kufikia mshahara wake, ambao ni zaidi ya pauni 300, 000 kwa wiki.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba wachezaji wenzake na Sancho wa England akiwamo Harry Maguire, Marcus Rashford na Luke Shaw walimtaka Sancho kuomba msamaha ili kurejea kwenye timu, lakini bado hajafanya hivyo.

BISSAKA KUFUNGWA UPYA

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 738,

MECHI KALI
GREEN BUFFALOES
VERSUS
POWER DYNAMOS
1 | 2.12
X | 3.03
2 | 3.23

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# STERLING ATAKIWA KUMSHAWISHI SOUTHGATE



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino, amemtaka Raheem Sterling kuwa na muendelezo katika kiwango chake bora ili kumdhihirishia Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, kuwa alikosea kumweka nje ya kikosi chake.

Sterling alihusika katika mabao yote manne yaliyofungwa na Chelsea wakati ikiibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Burnley baada ya kuwa nyuma kabla ya kuibuka na ushindi.

Mkongwe huyo aliyecheza mechi 82, kwa mara ya mwisho aliichezea England katika fainali zilizopita za Kombe la Dunia na aliachwa nje ya kikosi mara nne mfukulizo katika mechi za kirafiki pamoja na Australia na mechi ya kufuzu kwa Euro 2024 dhidi ya Italia.

"Nafikiri kutokana na uzoefu wake najua anahitaji kucheza na kumuonesha kocha wa timu ya taifa kuwa alikosea kufanya uamuzi wake," alisema Pochettino baada ya Chelsea kufunga mabao manne katika Ligi Kuu kwa mara ya kwanza tangu Aprili mwaka 2022.

"Kiwango na kufunga mabao ndio vitu pekee ambavyo vinaweza kuonesha kuwa mchezaji huyo bado anafaa kuwamo katika kikosi hicho cha taifa."

Chelsea, wakiongozwa na Sterling, baadaye walifunga mara tatu katika kipindi cha pili chenye nguvu na kuondoka na pointi zote tatu.



## Davies azigonganisha Man City, Madrid

**LONDON,** England

KLABU ya Manchester City imeingia vitani dhidi ya Real Madrid kuwania saini ya beki wa pembeni wa Bayern Munich na Canada, Alphonso Davies, katika dirisha dogo la Januari.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 22, mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika mwaka 2025.

Hata hivyo, Davies ameonesha nia ya kutohitaji kusaini mkataba mpya na kusisitiza kwamba anataka kupata changamoto mpya sehemu nyingine.

Munich inafahamu ikiwa itashindwa kumshawishi Davies, itatakiwa kumuuza dirisha lijalo la majira ya joto, kwani ikisubiri hadi Januari 2025 itakuwa kwenye presha ya kumpoteza bure ama kumuuza kwa kiasi kidogo cha fedha.

Hadi sasa, Davies amecheza mechi 10 kwenye michuano yote na kutoa asisti tatu.

Na amekuwa akisifika kwa uwezo wake mkubwa wa kupandisha mashambulizi kwa kasi na mashabiki wa soka Ujerumani wamembatiza jina la utani la Pikipiki.

,772,220

# MWAKINYO AFUNGIWA NGUMI MWAKA MMOJA NA FAINI JUU

Na Shufaa Lyimo

KAMISHENI ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), imemfungia Bondia Hassan Mwakinyo kujihusisha na mchezo wa ngumi nje na ndani ya nchi kwa muda wa mwaka mmoja pamoja na faini ya shilingi milioni moja baada ya kugomea pambano lake la kimataifa lililokuwa lifanyike Septemba 29, mwaka huu dhidi ya mpinzani wake Julius Indongo kutoka Namibia.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Kamisheni hiyo George Silas, alisema maamuzi hayo yametolewa na Kamati ya Nidhamu ya TPBRC ambayo ilikaa Oktoba 5, mwaka huu.

**Alisema walikaa na kuzungumza na pande zote mbili na kubaini kuwa vielelezo na maelezo ya Mwakinyo hayakuwa na sababu zenye mashiko, hivyo kulazimika kumpa adhabu hiyo.**

“Mwakinyo amepewa adhabu hiyo baada ya kuonekana kukiuka taratibu za mkataba wake dhidi ya Paf Promotion chini ya Godson Karigo,” alisema Silas.

Katibu huyo aliongeza kuwa mbali na adhabu hizo vile vile anaruhusiwa kukata rufani ndani ya siku saba kuanzia jana.

Aliongeza kuwa wamelazimika kutoa maamuzi hayo kwa kuwa Mwakinyo ni bondia mkubwa ambaye hakupaswa kufanya kitendo kama hicho.

“Wakati tulipokuwa tunazungumza nao wote wawili, alimtupia maneno makali mmoja wa kiongozi aliyekuwapo kwenye kikao kitendo kilichoonesha utovu wa nidhamu, hivyo kulazimika kumpa adhabu hiyo ili iwe fundisho kwa wengine,” alisema.

Wakati huo huo, Mkurugenzi wa Paf Promotion, Karigo alisema baada ya kamisheni hiyo kutoa maamuzi hayo, watakutana hivi karibuni ili wajue jinsi gani watarudishiwa gharama zao walizozitumia.

“Kamisheni imefuata kanuni na taratibu zake ambazo hatuwezi kupingana nao, kwa upande wetu tutakutana na kutoa maamuzi yetu ambayo tutawaeleza baada ya kikao chetu,” alisema Karigo.

Mwakinyo ambaye Septemba 29, mwaka huu, alikuwa apande ulingoni jijini Dar es Salaam dhidi ya Indongo, mapema asubuhi ya siku ya pambano hilo alitoa taarifa kupitia mitandao ya kijamii kuwa hatacheza pambano hilo kutokana na kukiukwa kwa makubaliano.

## MCHANGANI...




Watoto wakicheza mpira katika viwanja vya Jakaya Kikwete, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga hakuna kulala

INATOKA UKURASA 24

Yanga, Miguel Gamondi, ameshaanza kuifungia kazi Azam kwa kuangalia mikanda ya video ya timu hiyo ilivyocheza mechi zake za Ligi Kuu msimu huu ili kung'amua ubora na udhaifu wa timu hiyo, hivyo alisema anahitaji muda mrefu wa kuwa na wachezaji ili kuwatengeneza kuweza kudhibiti ubora wa wapinzani wao na kuutumia udhaifu wao kwa ajili ya kupata ushindi kwenye mechi ijayo.

Yanga inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa ikiwa na pointi 12 kwa mechi tano ilizocheza mpaka sasa, ikishinda mechi nne na kupoteza moja.

## *Simba yatawanyika, Al Ahly yajifungia*

INATOKA UKURASA 24

hayo na nguvu zetu ni katika mchezo huo ujao dhidi ya Al Ahly, si wageni kwetu, tuliwafunga kwa Mkapa, tunahitaji kuendelea tulipoishia na kwenda kupata matokeo chanya kwenye mechi ya marudiano nchini Misri,” alisema Kajula.

Aidha, Kajula alisema kabla ya kuanza kwa michuano ya Afrika Football League hasa kwenye mechi yao dhidi ya Al Ahly Oktoba 20, wiki hii wanakuja na jambo kubwa ‘Suprise’ kuelekea kwenye sherehe za ufunguzi.

Licha ya kutoweka wazi ni jambo gani, lakini kuna habari za ndani zinasema kuwa ni suala la utambulisho mkubwa wa jezi watakazotumia katika michuano hiyo.

## JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 11/10/23 | 23:15 | Bogota vs Cortulua | 2.14 | 3.01 | 3.32 |
| 2. 11/10/23 | 23:15 | Real Soacha vs Real Santander | 2.39 | 3.01 | 2.86 |
| 3. 12/10/23 | 02:15 | Deportivo Cali vs Deportes Tolima | 2.33 | 2.96 | 3.01 |
| 4. 12/10/23 | 04:05 | Tapatio vs Leones Negros | 2.15 | 3.26 | 3.05 |
| 5. 12/10/23 | 17:00 | Azerbaijan U21 vs Northern Ireland U21 | 2.79 | 3.20 | 2.33 |
| 6. 12/10/23 | 19:00 | Russia vs Cameroon | 2.27 | 3.23 | 3.23 |
| 7. 12/10/23 | 19:00 | Slovakia U21 vs Poland U21 | 2.37 | 3.20 | 2.74 |
| 8. 12/10/23 | 21:45 | Albania vs Czech Republic | 3.22 | 3.17 | 2.30 |
| 9. 13/10/23 | 17:00 | Greece U21 vs Croatia U21 | 2.70 | 3.05 | 2.36 |
| 10. 13/10/23 | 19:00 | Estonia vs Azerbaijan | 2.21 | 3.12 | 3.49 |
| 11. 13/10/23 | 21:45 | Austria vs Belgium | 2.70 | 3.28 | 2.60 |
| 12. 13/10/23 | 21:45 | Ireland vs Greece | 2.43 | 3.11 | 3.06 |
| 13. 13/10/23 | 22:00 | Real Oviedo vs Albacete | 2.31 | 2.88 | 3.23 |

## MECHI ZA USHINDI

“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 11/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4836 | Yokohama F Marinos vs Urawa Red Diamonds | 1.97 | 3.57 | 3.21 |
| 14:30 | 2025 | Bialystok Youth vs Lech Poznan Youth | 2.35 | 4.03 | 2.35 |
| 15:00 | 2448 | Wigan U23 vs Crewe U21 | 1.31 | 5.48 | 6.50 |
| 15:00 | 3672 | Rakow Czestochowa U19 vs Legia Youth | 2.31 | 4.02 | 2.39 |
| 16:00 | 1058 | Anagennisi Karditsas vs Eolikos Myt | 1.93 | 3.05 | 3.92 |
| 16:00 | 1234 | Niki Volou vs Levadiakos | 2.95 | 2.90 | 2.27 |
| 16:00 | 1798 | Kozani FC vs Makedonikos FC | 2.26 | 3.04 | 3.04 |
| 16:00 | 1970 | FK Panevezys B vs FA Siauliai B | 1.98 | 3.92 | 2.86 |
| 16:00 | 2502 | Green Buffaloes vs Power Dynamos | 2.12 | 3.03 | 3.23 |
| 16:00 | 3778 | Unicov vs Zlin | 5.09 | 4.02 | 1.53 |
| 16:00 | 4196 | Germany U19 vs Kazakhstan U19 | 1.03 | 11.21 | 25.48 |
| 16:00 | 4381 | Bsk Bijelo Brdo vs NK Vukovar 91 | 2.77 | 3.18 | 2.30 |
| 16:00 | 4720 | Povazska Bystrica vs Tatran Presov | 3.05 | 3.40 | 2.09 |
| 16:00 | 4842 | AE Larissa vs PO Triglias | 1.93 | 3.15 | 3.76 |
| 16:00 | 4870 | Diagoras FC vs Panetolikos | 5.09 | 3.77 | 1.57 |
| 16:00 | 5975 | Finland U19 vs Romania U19 | 3.10 | 3.40 | 2.07 |
| 16:05 | 1393 | Rustaq Club vs Al Nasr Salalah | 2.29 | 2.70 | 3.41 |
| 16:10 | 5582 | Al Nahda (Oman) vs Oman Club | 1.77 | 3.10 | 4.30 |
| 16:30 | 1090 | FC Kolin vs Bohemians | 10.15 | 6.90 | 1.17 |
| 16:30 | 5008 | Brinje Grosuplje vs NK Nafta | 2.10 | 3.34 | 2.98 |
| 17:00 | 4660 | AL Tora vs Al-Yarmouk | 2.85 | 3.06 | 2.37 |
| 17:30 | 4265 | Denizlispor vs Burhaniye Bld | 1.15 | 6.55 | 13.31 |
| 18:40 | 3111 | Al Seeb vs Sur | 1.78 | 3.22 | 4.40 |
| 19:00 | 5778 | FK Viktoria Zizkov vs Sigma Olomouc | 5.09 | 4.02 | 1.53 |
| 19:30 | 1097 | Kopparbergs Go W vs Twente W | 3.65 | 3.80 | 1.72 |
| 20:00 | 2296 | Afjet Afyonspor vs Adana 1954 FK | 1.47 | 4.02 | 5.91 |
| 20:30 | 2631 | FC Altona 93 vs SV Rugenbergen | 1.13 | 7.71 | 12.17 |
| 20:30 | 4680 | Le Mans vs FC Rouen | 2.18 | 3.10 | 3.30 |
| 20:30 | 5750 | Avranches vs FC Martigues | 2.80 | 3.26 | 2.37 |
| 20:30 | 5845 | CD Pradejon vs Atletico Lugones | 1.85 | 3.67 | 3.67 |
| 21:00 | 3500 | Desportivo Brasil U20 vs Mirassol FC U20 | 4.29 | 4.04 | 1.61 |
| 21:00 | 4301 | FC Zurich W vs Ajax W | 8.74 | 4.88 | 1.28 |
| 21:00 | 4487 | Corinthians SP U20 vs EC Agua Santa SP U20 | 1.54 | 3.93 | 5.10 |
| 21:45 | 1052 | Messina FC vs Casertana | 2.61 | 3.13 | 2.72 |
| 21:45 | 2929 | Wales vs Gibraltar | 1.08 | 9.29 | 42.23 |
| 21:45 | 5160 | Gosport Borough vs Dorchester Town | 1.41 | 4.66 | 5.68 |
| 21:45 | 5624 | ASD Pineto Calcio vs Pescara Calcio | 3.35 | 3.55 | 1.85 |
| 22:00 | 1194 | CD Ceuta 6 de Junio vs CD Bunol | 5.57 | 3.87 | 1.55 |
| 22:00 | 1537 | Dijon vs Epinal | 1.68 | 3.46 | 4.96 |
| 22:00 | 1772 | Cholet vs Orleans | 2.20 | 3.10 | 3.25 |
| 22:00 | 2445 | Villefranche Sur Saone vs FC Goal | 1.91 | 3.24 | 3.97 |
| 22:00 | 2590 | Nancy vs Red Star | 3.10 | 3.10 | 2.27 |
| 22:00 | 4682 | Chateauroux vs Sochaux | 2.29 | 2.95 | 2.90 |
| 22:00 | 5611 | US Marignane vs Nimes | 2.74 | 3.05 | 2.55 |
| 22:00 | 5874 | Niort vs FC Versailles 78 | 2.28 | 3.09 | 3.09 |
| 23:00 | 3187 | Guayaquil SC vs Cuniburo FC | 2.39 | 3.10 | 2.79 |
| 23:15 | 3581 | Llaneros FC vs Cucuta Deportivo | 2.02 | 3.05 | 3.61 |
| 23:15 | 4172 | Bogota FC vs Club Cortulua | 2.11 | 3.10 | 3.31 |
| 23:15 | 5471 | Deportes Quindio vs Universitario Popayan | 1.52 | 3.85 | 5.47 |
| 23:15 | 5849 | Patriotas FC vs Tigres FC (COL) | 1.40 | 4.03 | 7.34 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Oktoba 11, 2023

Nipashe




Sancho kuondoka Man Utd UKURASA 21

# Simba watawanyika, Al Ahly wajifungia AFL

●●● Mastaa hakuna kwenda timu za taifa, kutua nchi siku Wekundu wa Msimbazi wakiingia kambini...

**Na Saada Akida**

WAKATI wachezaji wa Simba wakitawanyika juzi kwenda mapumzikoni huku walioitwa kwenye timu zao za taifa wakiruhusiwa kwenda kujiunga nazo, hali ni tofauti kwa wapinzani wao wa michuano ya African Football League (AFL), Al Ahly ya Misri, baada ya kuamua kujifungia kambini na wachezaji wao wote.

**Licha ya wachezaji wengi wa Al Ahly kuunda kikosi cha Timu ya Taifa ya Misri kinachotarajiwa kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Namibia jijini Cairo, wachezaji wote wa klabu hiyo hawatajiunga na timu zao za taifa ili kuingia kambini kujiandaa na mechi hiyo dhidi ya Simba.**

Nyota wengine akiwamo mshambuliaji Percy Tau wa kikosi cha kwanza cha Timu ya Taifa ya Afrika Kusini na kiungo mkabaji Aliou Dieng ambaye ni panga pangua ndani ya timu yake ya Mali, taarifa zinaeleza wote wametakiwa kuwa kambini kuelekea mchezo huo wa ufunguzi wa AFL dhidi ya Simba Oktoba 20, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Al Ahly inatarajiwa kutua nchini Oktoba 17, mwaka huu, tayari kwa mechi hiyo, siku ambayo ndiyo Simba itaanza kujikusanya kuingia kambini.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Iman Kajula, alisema baada ya kufanikiwa kuvuna alama sita ugenini sasa akili na nguvu zao zinaelekezwa kwenye michuano AFL kuhakikisha wanashinda mechi yao ijayo dhidi ya Al Ahly.

Alisema baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Singida Fountain Gate, kikosi chetu kimerejea Dar es Salaam huku wachezaji wakipewa mapumziko.

"Kwa sasa tuko kwenye mapumziko ya Kalenda ya FIFA ambayo yameanza Oktoba 9 hadi 17, mwaka huu, hivyo Ligi itasimama kupisha mechi za timu za taifa kwa hiyo katika kipindi hiki wachezaji watapumzika na walioitwa timu zao za taifa wameruhusiwa kwenda kujiunga nazo kutumikia mataifa yao.

"Baada ya ratiba ya Kalenda ya FIFA kumalizika, kikosi kitarejea haraka kambini kujiandaa na mchezo wa ufunguzi wa African Football League dhidi ya Al Ahly utakaopigwa Oktoba 20," alisema Kajula.

Aliongeza kuwa kocha Robertinho Oliveira, anafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza mechi zilizopita kwa ajili ya kujiandaa na michuano hiyo kuhakikisha wanamfunga mpinzani wao huyo.

"Tumekuwa na mipango ya kila mechi, wakati tunaenda Mbeya na Singida malengo yetu yalikuwa kuchukuwa alama tatu kwa kila mchezo, tukafanikiwa kwa Tanzania Prisons na Singida Fountain Gate FC.

"Sasa tunasahau matokeo

INAENDELEA UKURASA 23



# SABABU MWAKINYO KUFUNGIWA NGUMI MWAKA NDANI, NJE

Hassan Mwakinyo

## Yanga hakuna kulala, tizi tu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu zingine zikitoa mapumziko ya siku kadhaa kwa wachezaji wake kutokana na mapumziko ya Kalenda ya FIFA, kikosi cha wachezaji wa Yanga ambao hawakuitwa kwenye timu zao za taifa kitaendelea na mazoezi kama kawaida kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC, Oktoba 25.

Meneja wa klabu hiyo, Walter Harrison, amesema kuwa wachezaji wote wa timu hiyo ambao hawajachaguliwa kwenye vikosi vya Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kwa wachezaji wazawa na timu za mataifa mengine wataendelea na 'program' ya mazoezi kama kawaida kwa sababu wana mchezo mgumu dhidi ya Azam FC.

"Tuna wachezaji 11 ambao wataondoka kwenda kuzitumikia klabu zao za taifa, kuna wachezaji wa Tanzania, Mali, Uganda, Burkina Faso, wataelekea kuziwakilisha nchi zao, lakini wale ambao hawajaitwa kwenye timu yoyote ya taifa watakuwa hapa hapa nchini kwa ajili ya 'program' za mazoezi kujiandaa na mchezo utakaofuata dhidi ya Azam FC Oktoba 25 kama hakutokuwa na mabadiliko ya ratiba, na mazoezi yataendelea hadi hapo waliokwenda kwenye timu za taifa watakaporejea, wataungana na wenzao hapo sasa tutakuwa tuna kikosi kamili kwa ajili ya mechi yetu inayofuata.

Wachezaji wa nje ambao wanatarajia kwenda kwenye vikosi vya timu ya taifa ni Khalid Aucho akienda kuichezea timu yake ya Uganda Cranes, Stephane Aziz Ki, akienda kulitumikia taifa lake la Burkina Faso na Djigui Diarra anayerejea kuidakia timu yake ya Taifa ya Mali, huku waliosalia ambao ni wazawa, watakwenda kwenye kikosi cha Taifa Stars.

Tayari Kocha Mkuu wa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >